# HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA MHESHIMIWA CHARLES N. KEENJA (MB.), KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA 2002/2003

## I. UTANGULIZI

**1.** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kisekta ya Uzalishaji Mali inayohusu Wizara ya Kilimo na Chakula, na baada ya kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja, kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2002/2003.

**2.** Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na wasemaji walionitangulia kutoa salaam za rambirambi kwako Mheshimiwa Spika na kwa Bunge lako Tukufu kutokana na vifo vya Marehemu Sebastian R. Kinyondo, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini na Marehemu John F. Mangwangwa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mpanda Magharibi. Kwa niaba ya Wizara yangu, Wananchi wa Jimbo langu la Ubungo na kwa niaba yangu binafsi, natoa pole kwa familia za marehemu na wananchi wa Majimbo hayo. Napenda pia kutoa salamu za rambirambi kwa ndugu na jamaa wa aliyekuwa Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali, Marehemu Sigfrid Lushagara na kwa ndugu na jamaa wa Maafisa wa Serikali wakiwamo, Maafisa 28 wa Kilimo waliofariki katika kipindi hiki.

**3.** Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Taifa letu limepatwa na ajali mbaya za barabarani, ajali ya tela la trekta iliyotokea Arumeru, ajali iliyotokea kwenye mgodi wa Mererani ya tarehe 18 Juni, 2002, kuzama kwa kivuko cha Kilombero tarehe 11 Aprili, 2002 na ajali mbaya sana ya gari moshi iliyotokea tarehe 24 Juni, 2002. Kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Ubungo na kwa niaba ya Wizara ya Kilimo na Chakula nachukua nafasi hii kumpa pole Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Benjamin William Mkapa, wafiwa na wananchi wote wa Tanzania. Aidha, nampongeza Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Serikali kwa jumla na Waheshimiwa Wabunge kwa hatua madhubuti zilizochukuliwa kushughulikia ajali hizo. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi na atunusuru na ajali kama hizi siku zijazo.

**4.** Mheshimiwa Spika, viongozi wetu wakuu wa kitaifa wamekipa hadhi na msukumo wa pekee kilimo kwa kushiriki kikamilifu katika mikutano mbalimbali. Katika mikutano hiyo, viongozi wetu wameshirikiana na wadau wa sekta ya kilimo kupitia mafanikio na matatizo ya kilimo na kuainisha mikakati ya kuyakabili. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alupolihutubia Bunge tarehe 30 Januari, 2002 alikipa Kilimo umuhimu mkubwa na pia aliongoza mkutano wa wadau wa zao la mkonge tarehe 25 Agosti, 2001 na alifungua mkuatano wa mwaka wa wadau wa zao la korosho tarehe 29 Septemba, 2001. Aidha, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, (Mb) aliongoza mikutano ya wadau wa sekta ndogo za tumbaku (Desemba 2001), kahawa (Machi 2002) na pamba (Aprili 2002). Napenda kuwashukuru kwa dhati viongozi hao kwa kutoa maelekezo thabiti ya kuleta mapinduzi ya kilimo nchini.

**5.** Mheshimiwa Spika, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, aliongoza ujumbe wa Tanzania katika Mkutano wa Chakula Duniani uliofanyika Roma, Italia tarehe 10 – 13 Juni, 2002. Mkutano huo ulifanya mapitio ya maendeleo ya utekelezaji na mpango wa kupunguza idadi ya watu wenye njaa duniani na kuweka mikakati mipya ya kufikia malengo hayo. Aidha, viongozi wa nchi katika mkutano huo walitoa tamko liitwalo *"Kuunganisha Nguvu Kupiga Vita Njaa"*. Tofauti na vilivyodai vyombo vya habari vya Magharibi, mkutano huo ulipata mafanikio makubwa, pengine kuliko ilivyotarajiwa.

**6.** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kisekta ya Uzalishaji Mali na Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati hiyo, kwa kuchambua kwa makini taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Mwaka wa 2001/2002 na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Mwaka wa 2002/2003 ya Wizara ya Kilimo na Chakula. Waheshimiwa Wabunge wa kamati hiyo walisisitiza umuhimu wa kujenga na kuimarisha miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji maji mashambani ili kuimarisha uhakika wa chakula nchini na kupunguza umaskini. Aidha, walishauri Wizara kutoa kipaumbele katika upatikanaji wa mikopo kwa wakulima, uimarishaji wa mfuko wa pembejeo, uenezaji wa kilimo kinachotumia wanyama kazi na uendelezaji wa mazao mbadala. Ushauri, maoni na maelekezo yaliyotolewa na kamati yamezingatiwa katika mapendekezo ninayowasilisha mbele ya Bunge hili tukufu na yataendelea kuzingatiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara siku hadi siku.

**7.** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo na Chakula Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mbunge wa Namtumbo, Bwana Wilfred Ngirwa, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara za Wizara na Asasi zilizoko chini ya Wizara, Watumishi wote na Wadau wa Sekta ya Kilimo kwa ushirikiano na ushauri wao katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2002. Napenda pia kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara na Asasi zake, ambao chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wamechangia kwa njia mbalimbali katika kuandaa taarifa ya utekelezaji ya mwaka wa 2001/2002 na makisio ya mapato na matumizi ambayo nina heshima kuyawasilisha mbele ya Bunge hili Tukufu. Nawashukuru wote kwa dhati kabisa.

**8.** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye (Mb.), Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba (Mb.), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Abdallah Kigoda (Mb.), kwa hotuba zao nzuri ambazo zimechambua na kufafanua masuala mengi ya kiuchumi na ya kijamii, ikiwa ni pamoja na hali ya kilimo na chakula nchini na hatua tunazochukua kukifanya kilimo kikue kwa kasi kubwa zaidi. Wakati wa kujadili hotuba hizo, Waheshimiwa Wabunge walitoa michango mizuri sana ya ushauri na mawazo ambayo tuliyachukua na tutayafanyia kazi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa uelewa wao wa sekta ya kilimo na kwa ushirikiano wao katika kuhimiza ukuaji wa sekta hiyo.

## II. HALI YA KILIMO NCHINI

**9.** Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kuanzia mwaka wa 1999 hadi mwaka wa 2001, sekta ya kilimo ilikua kwa wastani wa asilimia 3.7 kwa mwaka, ikilinganishwa na ongezeko la watu la asilimia 2.8 kwa mwaka. Ukuaji huo bado ni mdogo na usioridhisha na unatokana na uwekezaji mdogo katika sekta ya kilimo, matumizi ya teknolojia duni, matumizi madogo ya zana bora za kilimo, milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao, kushuka kwa bei za mazao makuu ya biashara, kilimo kutegemea sana mvua, kuvurugika kwa utaratibu wa kuagiza na kusambaza pembejeo na wakulima kutokuwa na uwezo wa kununua pembejeo za kutosha na athari za janga la UKIMWI. Matatizo haya, kwa sehemu kubwa, ndiyo yanayosababisha kutokufikiwa kwa tija inayowezekana katika kilimo (*Kiambatanisho Na.1*).

**10.** Mwaka wa 2001, sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 5.5 ikilinganishwa na asilimia 3.4 mwaka wa 2000. Katika ukuaji huu, mchango wa mazao ulikuwa asilimia 3.9, mifugo asilimia 0.8, misitu na uwindaji asilimia 0.3 na uvuvi asilimia 0.5. Ukuaji huu ulitokana na ongezako la uzalishaji wa mazao, hasa mazao ya chakula uliofikia asilimia 5.9 ikilinganishwa na asilimia 2.9 tu katika mwaka wa 2000. Katika miaka ijayo, sekta ya kilimo inatarajiwa kukua kwa kasi kubwa zaidi kutokana na uwekezaji unaotarajiwa kufanywa katika maeneo yanayomnufaisha mkulima moja kwa moja, kuruhusiwa kwa uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi, ushindani wa soko huria, uimarishaji wa huduma za ugani na uhamasishaji wa wakulima katika ngazi zote. Katika ukuaji huo, mazao yanategemewa kuchangia zaidi ya asilimia 75 ya ukuaji ikilinganishwa na mchango wa asilimia 70 ya ukuaji wa mwaka wa 2001.

## Hali ya Chakula Nchini katika Mwaka wa 2001/2002

**11.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002 Taifa lilikuwa na jumla ya tani milioni 8.08 za mazao ya chakula kilichotokana na mavuno ya mazao ya msimu wa 2000/2001 ya tani milioni 7.69 zikiwemo tani milioni 4.14 za mazao ya nafaka na tani milioni 3.55 za mazao yasiyo nafaka. Aidha, msimu huo ulianza na albaki ya tani 390,000 ya msimu wa 1999/2000, ambayo ilitokana na tani 45,000 za Hifadhi ya Taifa ya Chakula, hifadhi ya wafanyabiashara binafsi ya tani 44,000 na akiba ya wakulima iliyokisiwa kuwa tani 271,000. Katika kipindi cha Januari hadi Mei, 2002 tuliuza nje ya nchi tani 239,045 za mahindi, tani 2,180 za maharage, tani 1,300 za ngano na tani 90 za mtama. Wakati huo huo, tuliagiza kutoka nje ya nchi tani 130,037 za ngano na tani 6,906 za mikunde.

## Matarajio ya Chakula Nchini katika Mwaka wa 2002/2003

**12.** Mheshimiwa Spika, tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula nchini kwa msimu wa 2001/2002 inaonyesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula utafikia tani milioni 8.55, zikiwemo tani milioni 4.44 za mazao ya nafaka na tani milioni 4.11 za mazao yasiyo nafaka. Makisio ya mahitaji ya chakula katika mwaka wa 2002/2003 yanatarajiwa kuwa tani milioni 8.38. Kwa hiyo, tunatarajia kujitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada ya tani 166,000 (*Kiambatanisho Na. 2A*). Aidha, inatarajiwa kwamba kutakuwepo albaki ya tani 379,000 ya mwaka wa 2001/2002 na hivyo kufanya kuwepo kwa ziada ya tani 544,000 za chakula. Takwimu hizi zinaonyesha kuwa hali ya chakula imeendelea kuwa nzuri ikilinganishwa na ilivyokuwa miaka miwili iliyopita (*Kiambatanisho Na. 2B na Na.2C*).

**13.** Pamoja na kuwapo kwa hali nzuri ya kujitosheleza kwa chakula kitaifa, kutakuwepo na maeneo machache katika baadhi ya mikoa ambayo yatakuwa na upungufu wa chakula. Mikoa hiyo ni pamoja na Arusha (Wilaya za Monduli na Ngorongoro), Manyara (Wilaya ya Simanjiro), Kilimanjaro (Wilaya za Same, Mwanga na Moshi Vijijini) na Tabora (Wilaya ya Igunga). Sababu kubwa ya kuwapo kwa upungufu wa chakula katika maeneo hayo ni mvua zilizonyesha kwa kiwango kidogo na kwa mtawanyiko mbaya. Maeneo hayo yatapata chakula kutoka kwenye maeneo yenye ziada na wananchi wa maeneo hayo wanashauriwa kujinunulia chakula mapema.

## Hali ya Chakula katika Nchi jirani

**14.** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), hali ya chakula katika nchi za Kenya, Uganda na Rwanda katika mwaka wa 2001/2002, itakuwa nzuri kutokana na nchi hizo kupata mvua za kutosha. Lakini, kutokana na vita na migogoro ya kisiasa inayoendelea katika nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, hali ya chakula katika nchi hizo itaendelea kuwa mbaya. Wakati huo huo, nchi nyingi za Kusini mwa Afrika, zikiwemo Malawi, Msumbiji, Zambia, Zimbabwe, Angola, Swaziland na Lesotho zimeathirika kwa ukame na hivyo zina upungufu mkubwa wa chakula. Tathmini ya awali ya chakula katika nchi za SADC imebaini kuwepo kwa upungufu wa mahindi unaokadiriwa kufikia tani milioni 3.67. Kutokana na hali hiyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alizipa nchi za Malawi na Zambia msaada wa tani 2,000, za mahindi kila moja katika mwaka huu.

**15.** Mheshimiwa Spika, kutokana na Tanzania kuzungukwa na nchi zenye upungufu wa chakula kwa upande wa magharibi na kusini, kuna dalili za bei za mazao ya chakula kupanda sana na kuwashawishi wananchi kuuza mazao waliyovuna msimu huu kwa wingi. Nachukua nafasi hii **kuwashauri wananchi kutenga chakula cha kutosheleza mahitaji ya familia zao hadi watakapokuwa na uhakika wa mavuno ya msimu wa 2002/2003**. Kwa wastani, mtu mmoja anahitaji kilo 237 za chakula kwa mwaka. Kwa hiyo, familia ya watu watano inahitaji kilo 1,185 za chakula kwa mwaka au magunia yasiyopungua 12. Aidha, wananchi wahimizwe kuendeleza kilimo cha kiangazi kwa kulima kwenye mabonde yenye unyevunyevu na kwa kumwagilia maji mashambani ili kuzidi kuimarisha usalama wa chakula katika

familia. Wafugaji nao, wanashauriwa kuuza sehemu ya mifugo yao na kujinunulia chakula cha kutosha mahitaji ya familia zao hadi mavuno ya msimu wa 2002/2003 wakati huu ambapo bei za chakula bado ziko chini.

**16.** Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa sana ya kilimo chetu inategemea mvua. Hata kule kwenye kilimo cha umwagiliaji maji mashambani, upatikanaji wa maji unategemea kuwepo kwa mvua za kutosha. Kwa kawaida, nchi yetu huwa na miaka ya mvua za kuridhisha ambayo hufuatiwa na vipindi vya mvua chache kwenye baadhi ya maeneo ya nchi. Nchi imepata mvua nzuri kwa miaka miwili mfululizo, 2000/ 2001 na 2001/2002. Wakati tukimwomba Mwenyezi Mungu atuzidishie neema, **inabidi tuchukue tahadhari ya kujiwekea akiba ya chakula ya kutosha katika ngazi ya familia na pia katika ngazi ya Taifa, hadi tutakapokuwa na uhakika wa mavuno ya msimu wa 2002/2003.** Hali mbaya ya chakula katika nchi za kusini mwa Afrika inapaswa kuwa fundisho kwetu.

## Mazao ya Biashara

**17.** Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2001/2002 uzalishaji wa mazao makuu ya biashara ambayo ni pamba, tumbaku, sukari, mkonge, chai na pareto uliongezeka kwa viwango tofauti. Uzalishaji wa pamba uliongezeka kwa asilimia 21, tumbaku kwa asilimia 13, sukari kwa asilimia 21, mkonge kwa asilimia 15 na pareto kwa asilimia 89. Uzalishaji wa chai uliongezeka kwa kiwango kidogo cha asilimia 2 tu. Ongezeko la uzalishaji wa mazao haya umetokana na uwekezaji unaoendelea, upatikanaji wa pembejeo, pamoja na hali nzuri ya hewa. Uzalishaji wa kahawa ulishuka kwa asilimia 38 na korosho kwa asilimia 45 kutokana na matatizo ya masoko (*Jedwali Na. 1*).

**18.** Bei ya zao la kahawa imeendelea kushuka wakati gharama za uzalishaji zimeendelea kupanda na hivyo kupunguza uwezo wa mkulima wa kununua pembejeo. Kwa mfano, wakati mahitaji ya madawa ya kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu yanayokadiriwa kufikia lita milioni mbili za madawa ya maji na tani elfu tano za madawa ya unga, wakulima wa kahawa nchini wanakadiriwa kutumia wastani wa lita 500,000 za madawa ya maji na tani 960 tu za madawa ya unga kwa mwaka. Hali hii inasababisha kahawa nyingi mashambani iharibiwe na magonjwa na wadudu na hivyo kusababisha kushuka kwa uzalishaji wa kahawa nchini.

**19.** Kwa zao la korosho, kushuka kwa uzalishaji kumesababishwa na matumizi madogo ya madawa ya kudhibiti ugonjwa wa "*ubwiri unga*", kutokana na wakulima kukosa fedha za kununulia pembejeo hizo baada ya kushuka kwa bei ya zao hilo katika msimu wa 2000/2001. (*Jedwali Na.1*).

*Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Mazao ya Biashara (Tani)*

| **ZAO** | **1999/2000** | **2000/2001** | **2001/2002** | **%Ongezeko 2000/2001** |
|---|---|---|---|---|
| Pamba | 105,853 | 123,558 | 149,091 | **21** |
| Tumbaku | 25,000 | 28,000 | 31,700* | **13** |
| Sukari | 116,927 | 135,534 | 163,994 | **21** |
| Mkonge | 20,600 | 20,500 | 23,540 | **15** |
| Chai | 23,979 | 26,386 | 26,848 | **2** |
| Pareto | 750 | 1850 | 3,500 | **89** |
| Kahawa | 47,811 | 58,134 | 36,175 | **-38** |
| Korosho | 121,207 | 122,283 | 67,369 | **-45** |

## III. UTEKELEZAJI WA KAZI NA MAFANIKIO KWA MWAKA WA 2001/2002

**20.** Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilipokuwa nikiwasilisha hotuba yangu bungeni, nileleza matatizo yanayofanya kilimo chetu kisiwe cha kisasa na chenye tija. Ufumbuzi wa mengi ya matatizo hayo upo ndani ya uwezo wetu. Katika kipindi cha mwaka wa 2001/2002 kazi kuu zilizofanyika katika kukabiliana na matatizo hayo ni pamoja na

- **Kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo**, *(Agricultural Sector Development Strategy)*, ikiwa ni hatua muhimu katika kutekeleza Mkakati wa Kuondoa Umaskini Kitaifa. Mambo muhimu yaliyopewa kipaumbele katika Mkakati huo ni pamoja na utafiti, huduma za ugani, kilimo cha umwagiliaji maji mashambani, hifadhi ya chakula, usindikaji wa mazao, matumizi ya pembejeo na zana bora, mikopo kwa wakulima, uimarishaji wa miundombinu, umuhimu wa jinsia katika kilimo na mapambano dhidi ya UKIMWI.
- Kukamilisha maandalizi ya Programu za kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agriculture sector Development Programme*) kwa kushirikiana na Wizara za Ushirika na Masoko, Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. **Halmashauri za wilaya nazo zinatakiwa kuandaa na kukamilisha programu za wilaya za kuendeleza kilimo kabla ya mwezi wa Oktoba, 2002** ili zizingatiwe katika makisio yao ya mwaka wa 2003.
- Kueneza na Kuendeleza mbinu mbalimbali za ugani zikiwepo **mbinu shirikishi jamii** ambayo imeleta mafanikio makubwa sana mkoani Singida na shamba darasa ambayo imekuwa na mafanikio katika wilaya za Kongwa, Kondoa, Kilosa, Kilombero, Morogoro Vijijini na Biharamulo.
- Kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao ambavyo visipodhibitiwa husababisha upotevu wa mazao unaokisiwa kufikia asilimia 30 hadi 40 kwa mwaka. Udhibiti huo ulihusu ndege aina ya kwelea kwelea, viwavijeshi, dumuzi, panya, nzige na magonjwa mbalimbali ya mimea. Aidha, Wizara iliendelea kueneza **mbinu za udhibiti husishi** ambazo zilileta mafanikio katika kudhibiti visumbufu vya mazao kama pamba, kahawa, mboga za majani, viazi vitamu, mahindi na muhogo.
- Kukamilisha utaratibu mpya wa kutoa mikopo ya pembejeo kutoka Mfuko wa Pembejeo za Kilimo wa Taifa kupitia kwenye mabenki.
- Kukamilisha skimu 27 za umwagiliaji maji mashambani zenye eneo lenye jumla ya hekta 9,578 kama ifuatavyo:
    1. Skimu 15 chini ya Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji maji mashambani;
    2. Skimu 11 chini ya Mradi wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji maji mashambani katika mabonde ya mito ya Pangani na Rufiji na
    3. Skimu ya Mwega, wilayani Kilosa.
- Kurekebisha mitaala ya vyuo vya kilimo, kutoa mafunzo rejea kwa maafisa ugani, wakulima na wataalam wa kilimo pamoja na kutayarisha aina nane za vitabu vya kiada na rejea.
- Kuendelea na zoezi la kubinafsisha mashirika ya umma yaliyo chini ya Wizara. Mashirika yaliyobinafsishwa ni Makao Makuu ya Shirika la Usagishaji la Taifa na Kampuni ya Sukari ya Kagera.
- Kukarabati viwanda viwili vya korosho vya Masasi na Kibaha na jineri nne za kuchambua pamba; Mwaya iliyoko Ulanga, Kilosa, Mandera iliyoko Bagamoyo na Korogwe.
- Kuendelea na utafiti wa mazao, hususan uzalishaji wa mbegu bora, mbinu bora za kilimo, uchunguzi wa udongo na mbinu za udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao. Mbegu bora aina tano za mahindi na mbili za mpunga zilitolewa na kuidhinishwa na Wizara.
- Kuunda mifuko ya kuendeleza utafiti katika kanda zote saba kwa kushirikiana na uongozi wa Mikoa, Wilaya na Serikali za Mitaa.

- Kupandisha vyeo viwili viwili watumishi 5,824 kati ya watumishi 6,865 waliostahili kupandishwa vyeo. Zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi wote hadi kufikia ngazi wanazostahili linaendelea.
- Kutathmini uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya chakula na biashara nchini.
- Kununua na kuweka akiba ya Hifadhi ya Chakula ya Taifa. Kutokana na akiba hiyo, Serikali ilitoa tani 4,000 za mahindi kama msaada wa chakula kwa Serikali za Malawi na Zambia.
- Kukamilisha sheria za Bodi za Sukari, Tumbaku, Kahawa na Pamba ambazo zimeanza kutumika mwezi wa Julai mwaka wa 2002.
- Kuendeleza matumizi ya zana bora za kilimo kwa kusambaza matrekta madogo ya mkono 170 mikoani na kutoa mafunzo kwa mafundi sanifu 105 na wakulima 7,090. Aidha, Wizara ilihamasisha sekta binafsi kuagiza na kusambaza nchini matrekta mapya na yaliyotumika.

## Maelezo kamili Zaidi Kuhusu kazi Zilizofanyika Katika Mwaka wa 2001/2002 ni Kama Ifuatavyo: -

### Mkakati wa Kuendeleza Kilimo

**21.** Mheshimiwa Spika, mwezi wa Agosti 2001, Serikali ilikamilisha maandalizi ya Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo, ikiwa ni hatua muhimu katika kutekeleza Mkakati wa Kuondoa Umaskini (PRS). Maandalizi ya programu za kutekeleza Mkakati huo yamekamilishwa na Wizara za Kilimo na Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Ushirika na Masoko na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Programu hizo zimeainisha maeneo ya kupewa kipaumbele ambayo yakitekelezwa, yatawezesha ukuaji wa kasi wa sekta ya kilimo. **Halmashauri za Wilaya zinatakiwa kuandaa programu zao za kuendeleza kilimo kuzingatia maeneo ya kipaumbele ya Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo**. Kwa kuzingatia Mkakati huo, Bodi za Mazao nazo zimekamilisha maandalizi ya mipango ya maendeleo ya mazao yaliyo chini ya Bodi hizo.

### Huduma za Ugani

**22.** Mheshimiwa Spika, mbinu **shirikishi jamii** (***Participatory Reflection Action – PRA***) ni njia ya kueneza teknolojia za kilimo bora na utoaji wa huduma za jamii kwa wakulima iliyoonyesha mafanikio makubwa katika maeneo ilikotumika na kutupa matumaini ya kupata ufumbuzi wa tatizo sugu la huduma za ugani kutokuwafikia wakulima. Mbinu hiyo huwawezesha walengwa kuibua matatizo yao, kuyachanganua, kupanga vipaumbele, kuainisha rasilimali zinazohitajika, kuandaa mipango ya utekelezaji, kutekeleza na kutathmini utekelezaji. Katika kutekeleza mbinu hiyo, Mkoa wa Singida umeandaa timu za wawezeshaji katika ngazi za Mkoa, Wilaya na Kata zinazoshirikisha viongozi na wataalam wa kilimo, mifugo, afya, maendeleo ya jamii, maliasili, elimu na ushirika. Kwa ujumla mbinu hiyo imeuwezesha mkoa wa Singida kuwa na mpango endelevu wa maendeleo na unaotumia kikamilifu nguvu kazi iliyopo katika mkoa. Aidha, mbinu hiyo imeweka bayana uwajibikaji wa viongozi katika kusimamia utekelezaji wa mpango ulioandaliwa katika mkoa huo.

**23.** Kwa kutumia mbinu hiyo, wananchi na uongozi wa mkoa wa Singida wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kutekeleza yafuatayo: -

- Kujitosheleza kwa chakula kwa misimu mitano kutoka mwaka wa 1997/1998 hadi 2002/2003,
- Kufanya sensa ya kaya na watu wote ili kubaini nguvu kazi iliyopo,
- Kutekeleza kwa asilimia 65 zoezi la kupima na kugawa mashamba kwa ajili ya kaya na vijana wenye umri wa miaka 18 na zaidi. Zoezi hili limebaini kuwapo kwa wananchi wasiokuwa na ardhi ya kutosha na hivyo kusadia uongozi kubuni utaratibu wa kuwapatia ardhi katika maeneo yenye ardhi ya kutosha,
- Kuongeza matumizi ya wanyama kazi hadi kufikia asilimia 95 kwenye baadhi ya tarafa na

kuongeza matumizi ya samadi na mbegu bora,

- Kuhakikisha kuwa wakulima wanapanda mazao yanayostawi vizuri katika mazingira yao na yanayopendekezwa kwa kanda yao ya kilimo.

Nawapongeza wananchi na viongozi wa mkoa wa Singida kwa mafanikio hayo. Uzoefu uliopatikana katika mkoa huo utaenezwa nchi nzima katika mwaka wa 2002/2003.

**24.** Wizara, kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), inaendeleza matumizi ya mbinu ya ugani iitwayo **Shamba Darasa *(Farmer Field School)*.** Shamba Darasa huundwa na wakulima 25 ambao huendeleza shamba la mfano kwa pamoja. Shamba hilo ndilo darasa. Siku za mafunzo wakulima hujigawa katika vikundi vya wakulima watano watano, kwa lengo la kufanya uchunguzi wa kina katika shamba la mfano, kuhusu hali ya mimea katika hatua mbalimbali za ukuaji, wadudu na magonjwa ya mimea yanayojitokeza. Baadaye wakulima huendesha majadiliano ya pamoja katika kikundi kizima cha wakulima 25 ili kuanisha teknolojia mbalimbali za kukabiliana na hali iliyojitokeza katika shamba la mfano. Baada ya mazao kukomaa, washiriki huwaalika wakulima wengine ili wajionee wenyewe mafanikio yaliyopatikana na kupata maelezo kuhusu mbinu zilizotumika kufanikisha uzalishaji. Katika msimu unaofuata kila mhitimu wa shamba darasa hutakiwa kuanzisha shamba darasa jingine likijumuisha wakulima wengine 24. Hivyo, chini ya utaratibu huu inawezekana wakulima wengi kijijini kufikiwa baada ya misimu kama mitatu hivi.

**25.** Katika mwaka wa 2001/2002, Wizara iliwezesha wakulima kuanzisha Mashamba Darasa 30 katika wilaya za Morogoro Vijijini, Kilosa, Kilombero, Kongwa, Kondoa na Biharamulo. Jumla ya wakulima 750 walishiriki katika mafunzo hayo. Kutokana na Mashamba Darasa, wakulima wamepata uwezo mkubwa wa kuchunguza matatizo ya kilimo na jinsi ya kuyatatua. Katika Mashamba Darasa, washiriki wameweza kuongeza maradufu mavuno ya mazao kwa hekta.

**26.** Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha usimamizi wa maafisa ugani, Serikali za Mitaa zilipewa jukumu la kusimamia mabwana shamba tangu mwaka wa 1998. Katika kipindi hicho, Wizara imebaini udhaifu katika mawasiliano na uhusiano kati ya Wizara na Mikoa na Serikali za Mitaa. Udhaifu huo unapunguza sana ufanisi wa shughuli za ugani katika Serikali za Mitaa na tumehakikishiwa kwamba suala hilo linatazamwa upya kwa lengo la kuondoa mapungufu yaliyopo na kuongeza ufanisi katika utendaji. Wizara imetoa mapendekezo kuhusu uimarishaji wa Sekretariati za Mikoa kwa kuongeza watendaji wa Sekta ya Kilimo ili kuongeza uwezo wa kutoa ushauri unaostahili katika masuala ya uendelezaji wa mazao, huduma za ugani, mafunzo kwa wakulima na watumishi, huduma za kifundi kama vile umwagiliaji maji mashambani, matumizi ya wanyama kazi na mashine katika kilimo, matumizi bora ya ardhi, udhibiti wa magonjwa na visumbufu vya mimea na ukusanyaji wa takwimu za kilimo. Ipo haja pia ya kufafanua mawasiliano na mipaka ya madaraka na wajibu kwa wote wanaohusika. Ni wajibu wa Serikali Kuu kusimamia Serikali za Mitaa na kuhakikisha kwamba zinatekeleza kikamilifu madhumuni na shabaha za kuzianzisha.

## Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea na Mazao

**27.** Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa 2001/2002, Wizara ikishirikiana na Serikali za Mitaa na wakulima, ilipambana na milipuko ya visumbufu mbalimbali vya mimea na mazao ikiwa ni pamoja na milipuko ya ndege waharibifu aina ya kwelea kwelea, viwavijeshi, panya, nzige na magonjwa mbalimbali ya mimea. Kila mwaka visumbufu hivi husababisha upotevu wa mazao unaokisiwa kufikia asilimia 30 hadi 40 ya mazao yote yanayozalishwa. Katika mwaka huu, Wizara ilifanikiwa kutuma wataalam mara taarifa za milipuko ya viumbe hao waharibifu zilipopokelewa na kwa kufanya hivyo, kupunguza sana malalamiko ya wakulima na uharibifu ambao ungeweza kutokea.

**28.** Mikoa 16 nchini ilikabiliwa na milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao kwa viwango tofauti. Kwelea kwelea walivamia mashamba ya nafaka katika mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma, Mbeya, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Mara na Iringa. Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Kilimanjaro na Pwani ilivamiwa na viwavijeshi. Zaidi ya hekta 9,000 za mashamba ya nafaka na malisho zilishambuliwa. Milipuko mikubwa ya panya ilitokea katika mikoa 13 nchini ambayo ni Arusha, Manyara, Tabora, Lindi, Singida, Morogoro, Pwani, Mbeya, Dodoma, Ruvuma, Mwanza, Shinyanga na Iringa. Visumbufu vingine vya mimea na mazao vilivyoendelea kuwa tishio nchini ni pamoja na nzige wekundu, dumuzi na ugonjwa wa batobato wa zao la muhogo. Visumbufu hivyo vimedhibitiwa kwa ufanisi kwa kutumia viuatilifu na mbinu za kibiolojia.

### Udhibiti wa ugonjwa wa mnyauko wa kahawa

**29.** Ugonjwa wa mnyauko wa kahawa kwa mara ya kwanza ulibainika katika Wilaya za Bukoba na Karagwe mkoani Kagera mwaka wa 2001. Ugonjwa huo husababishwa na kimelea aina ya "*Fusarium*" na ni wa hatari kwani husababisha mibuni iliyoshambuliwa kunyauka na kukauka. Ili kupunguza kasi ya kuenea kwa ugonjwa huu, Wizara imeweka utaratibu wa kudhibiti uingizaji na utoaji wa miche ya mibuni mkoani Kagera. Mbinu za uhakika za kuudhibiti ugonjwa huu ni kung'oa mibuni yote iliyoathirika, kuichoma moto na kupanda mbegu stahimilivu. Mbinu hizi zimeanza kutumika katika maeneo yaliyoathirika. Wizara imekamilisha utaratibu wa kuweka Mkoa wa Kagera chini ya karantini ya ungonjwa wa mnyauko wa kahawa. Chini ya karantini hiyo, ni marufuku kwa mtu yoyote kutoa mimea au sehemu yoyote ya mti wa kahawa nje ya mkoa wa Kagera isipokuwa kahawa iliyokobolewa. Aidha, mimea yote itakayobainika kushikwa na ugonjwa huu wa hatari ni lazima ing'olewe na kuchomwa moto mara moja.

### Udhibiti Husishi Wa Visumbufu Vya Mimea *( Integrated Pest Management IPM)*

**30.** Mheshimiwa Spika, udhibiti husishi ni matumizi ya njia mbalimbali za kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao kwa pamoja, ambazo ni njia za asili, kibiolojia, upandaji mimea stahimilivu na utumiaji wa viuatilifu inapokuwa ni lazima. Lengo kuu la mbinu hii ni kupunguza matumizi ya madawa na hivyo kupunguza gharama za uzalishaji, kuongeza tija, kulinda afya ya binadamu na mazingira. Katika mkoa wa Shinyanga, wakulima kwa kutumia mbinu hiyo, wameweza kupunguza minyunyizo ya madawa ya pamba kutoka minyunyizo sita hadi miwili kwa msimu na kuongeza mavuno ya pamba kutoka kilo 875 kwa hekta hadi kilo 1,500 kwa hekta. Aidha, wadudu mbalimbali maadui walisambazwa ili kudhibiti utitiri wa muhogo mkoani Morogoro.

### Kusimamia Sheria ya Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea ya Mwaka wa 1997

**31.** Mheshimiwa Spika, Sheria ya Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea ya mwaka wa 1997 ilianza kutumika tarehe 1 Julai, 2001. Kuanzia mwezi wa Julai, 2001 hadi Aprili, 2002, Wizara, kupitia taasisi ya *Tropical Pesticide Research Institute* (TPRI), ilichukua hatua za kudhibiti uingizaji wa madawa nchini ili kuhakikisha kuwa ni yale tu yaliyosajiliwa na yenye sifa za ubora zinazokubalika ndiyo tu yanaruhusiwa nchini. Kazi zilizofanyika chini ya sheria hii ni pamoja na kutoa vibali 291 vya uingizaji wa madawa kwa makampuni mbalimbali, kukagua shehena zote za madawa zilizoingizwa nchini na kutoa vyeti 2,731 vya usalama *(phytosanitary certificates).* Aidha, katika mazao yaliyokaguliwa, jumla ya tani 93,243 zilifukiziwa dawa ya kuua visumbufu vilivyogunduliwa na tani 2,022 ziliteketezwa kwa moto kwa kuwa zilikuwa na visumbufu hatari vya mazao.

### Udhibiti wa Gugumaji katika Ziwa Viktoria

**32.** Katika mwaka wa 2001/2002, udhibiti wa gugumaji uliendelea kwa kutumia njia za kibiolojia na kuopoa gugumaji kwa kutumia zana. Eneo la hekta 1,560 kati ya hekta 2,000 la mwambao wa ziwa lililokuwa limeathiriwa sana limesafishwa. Mbawakavu 56 milioni kwa ajili ya udhibiti wa gugumaji

kibiolojia walizalishwa na kusambazwa katika ghuba za Mwanza na Emilpasha, Mto Kagera na mwambao wa Rubavu. Pamoja na mafanikio haya, tatizo la gugumaji linaendelea kuwepo kutokana na kutodhibitiwa katika mto wa Kagera katika nchi ya Rwanda.

## Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani

**33.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002, Wizara ilitilia mkazo uanzishwaji wa miradi midogo, ya kati na mikubwa ya kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Kazi zilizofanywa ni pamoja na kukarabati skimu 15 zilizojengwa miaka iliyopita, kukamilisha ujenzi wa miradi 12, kueneza teknolojia rahisi za kilimo cha umwagiliaji maji mashambani, hususan uvunaji maji ya mvua na uchimbaji na ujenzi wa visima vifupi vya maji. Aidha, Wizara ilitoa kipaumbele kwa uanzishaji na uimarishaji wa vyama vya wamwagiliaji maji mashambani na kutoa mafunzo ya uendeshaji wa vyama hivyo kwa wakulima na maafisa ugani. Miradi ya Kilimo cha Umwagiliaji maji mashambani iliyotekelezwa kwa michango ya wakulima, serikali na wahisani mbalimbali ni kama ifuatayo:

## Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Programme Support - ASPS*)

**34.** Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Denmark na unaendelea kutekelezwa kwa kuendeleza skimu tano za kilimo cha umwagiliaji maji mashambani zenye jumla ya hekta 3,830. Katika mwaka wa 2001/2002, Wizara ilikamilisha upembuzi yakinifu wa skimu za Naming'ongo, Mbozi (hekta 1,000); Nyanzwa, Iringa Vijijini (hekta 760); Irindi, Iringa Vijijini (hekta 610) na Utengule Usongwe, Mbeya Vijijini (hekta 500). Usanifu wa mfumo na miundombinu katika skimu ya Lumuma, Kilosa (hekta 960) umekamilika na ujenzi umeanza.

## Mradi wa kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani katika mabonde ya Mto Pangani na Mto Rufiji (*River Basin Management and Smallholder Irrigation Improvement Project – RBMSIIP*)

**35.** Mradi huu ulioanza mwaka wa 1996 chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia, umekamilisha ujenzi wa skimu 11 zenye eneo la hekta 3,890 katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Iringa na Mbeya (*Kiambatanisho Na.3*). Familia 4,879 zimenufaika na ukamilishaji wa miradi hiyo. Wizara iliendelea kutoa huduma za ugani na kuimarisha vyama vya watumia maji kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya katika mikoa husika.

## Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani (*Participatory Irrigation Development Programme - PIDP*)

**36.** Programu hii ilianza kutekelezwa mwaka wa 2000 na itaendelea hadi mwaka wa 2,006. Programu inalenga kuendeleza hekta 7,200 za skimu za uvunaji maji katika wilaya 12 za mikoa 6 yenye mvua haba – Tabora (Nzega na Igunga), Dodoma (Dodoma Vijijini na Mpwapwa), Shinyanga (Shinyanga Vijijini), Singida (Iramba na Manyoni), Mwanza (Misungwi na Kwimba) na Arusha (Babati). Mradi huu unafadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Serikali ya Ireland na Mpango wa Chakula Duniani (WFP).

**37.** Katika mwaka wa 2001/2002, programu hiyo imekamilisha ukarabati wa skimu 15 zilizokuwa zimeharibiwa na mvua za El-Nino mwaka wa 1997/1998. Ukarabati huu umewezesha eneo la hekta 5,100 kulimwa ikilinganishwa na hekta 3,405 zilizolimwa msimu wa 2000/2001 sawa na ongezeko la asilimia 49.7. Skimu zilizokarabatiwa ni za Bahi, Chipokelo na Chipanga (Dodoma Vijijini); Lusilile, Saranda, na Chikuyu (Manyoni); Nata na Lusu (Nzega); Nduguti na Nsalala (Shinyanga Vijijini); Igongwa (Misungwi); Choma cha Nkola na Itumba (Igunga) na Tyeme-Masangi (Iramba). Aidha, programu

imechimba visima vifupi 130 vinavyotumia pampu za miguu (*Treadle pumps*) kwa ajili ya kumwagilia bustani za mboga na vitalu vya mbegu ya mpunga. Familia 5,036 zimenufaika na ukarabati uliofanywa.

### Maandalizi ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Kilimo cha Umwagiliaji maji Mashambani (*National Irrigation Master Plan Study*)

**38.** Mwaka wa 1994, Wizara iliandaa Mpango wa Kitaifa wa Maendeleo ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani (1994-2014) ambao unaendelea kutekelezwa. Aidha, katika miaka ya hivi karibuni, serikali imeandaa mikakati mbalimbali ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kama vile Mkakati wa Maendeleo Vijijini *(Rural Development Strategy)*, Mkakati wa Kupunguza Umaskini *(Poverty Reduction Strategy)* na Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Strategy).* Ili kuzingatia mwelekeo wa mikakati hiyo, Wizara inatayarisha Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani (*National Irrigation Master Plan).* Maandalizi ya mpango huo yanagharimiwa na Serikali za Tanzania na Japan. Mpango huo utaainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani na kupanga utekelezaji wake. Timu ya Wataalam wa Kijapani na Tanzania ilianza kazi ya kuandaa mpango huo mwezi wa Oktoba, 2001 na inatarajiwa kukamilika mwezi wa Machi, 2004. Taarifa zote muhimu za awali, zikiwemo taarifa za tafiti zilizofanywa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa, zinatumiwa katika utayarishaji wa mpango huo.

### Mradi wa Kuongeza Rutuba kwenye Udongo na Tija katika Kilimo (*Soil Fertility Recapitalization and Agricultural Intensification Project – SOFRAIP*)

**39.** Mheshimiwa Spika, ili kuleta maendeleo katika sekta ya Kilimo, Wizara imekamilisha maandalizi ya mradi wa miaka mitano wa kuongeza rutuba ya udongo na tija katika kilimo. Mradi huu unalenga kuondoa vikwazo vinavyowanyima wakulima fursa na uwezo wa kufikia kiwango cha juu katika ufanisi wa kilimo. Katika kutekeleza malengo ya mradi huo, wakulima watawezeshwa, kwa kutumia mbinu shirikishi, kutambua na kuchambua matatizo yao na baadaye kupanga na kutekeleza miradi yao ya maendeleo.

**40.** Katika kipindi cha mwaka wa 2001/2002, kazi kubwa iliyofanyika ni kutayarisha maandiko yote muhimu (key project documents), pamoja na kuanza kushirikiana na baadhi ya wilaya katika kusaidia vijiji vilivyoteuliwa na wilaya kutayarisha miradi itakayotekelezwa na jamii ya wakulima. Kazi hii imekwenda sambamba na utayarishwaji wa timu za wilaya katika mbinu shirikishi zinazoweza kuibua miradi ya kuendeleza kilimo (*Community Agriculture Investment Subprojects*). Wilaya zitakazoshiriki katika mwaka wa 2002/2003 ni Iringa, Morogoro, Singida, Hanang, Arumeru, Hai, Masasi na Nachingwea. Mafunzo muhimu yamefanyika kuandaa timu za wilaya zitakazowezesha vijiji kutayarisha miradi itakayoongeza tija na mapato katika kilimo.

Maandalizi ya mradi huu yamekuwa ya polepole sana. Waziri Mkuu alipoomba msaada wa Benki ya Dunia alitumaini kwamba ungepatikana haraka, ili upunguze matatizo ya mkulima. Pamoja na Waziri Mkuu kufuatilia maendeleo ya mradi huu mwenyewe na kuahidiwa kwamba mambo yangeharakishwa, bado maandalizi yamekuwa ya polepole sana.

### Hifadhi ya Udongo na Maji

**41.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002 Wizara ilitoa mafunzo kwa Maafisa Ugani 50 kutoka mikoa 11 ya Dodoma, Arusha, Tabora, Kilimanjaro, Shinyanga, Singida, Mwanza, Morogoro, Iringa, Rukwa, na Mbeya. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuandaa timu za wataalamu ambazo zitatoa mafunzo ya mbinu bora za kuhifadhi udongo na maji kwa wataalam wengine na wakulima katika mikoa hiyo *(Training of Trainers).* Chini ya Mradi wa kusimamia Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Viktoria,

(*Lake Victoria Environment Management Programme*) Wizara ilitumia picha za '*Satelite*' kubaini maeneo yaliyoathirika na mmomonyoko wa udongo katika mikoa ya ziwa, kwa lengo la kuyakarabati.

### UPATIKANAJI WA PEMBEJEO NA ZANA ZA KILIMO

## Mbolea na Madawa

**42.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002 makadirio ya mahitaji ya mbolea yalikuwa tani 185,500. Hadi kufikia mwezi wa Juni 2002 tani 145,067 zilipatikana, sawa na asilimia 78 ya mahitaji. Ili kutathmini upatikanaji wa mbolea na madawa, Wizara ilifanya mikutano miwili na waagizaji na wasambazaji wa pembejeo ambapo wadau 40 walishiriki. Kutokana na mikutano hiyo ilibainika kuwa mahitaji ya madawa ya maji yalikuwa lita milioni 4.6 na ya unga yalikuwa tani 24,000. Aidha upatikanaji wa madawa hayo ulikuwa lita milioni 1.6 za madawa ya maji na tani 12,000 za madawa ya unga.

## Zana za Kilimo

**43.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002 jumla ya matrekta makubwa 375, matrekta madogo ya mkono 46, majembe ya kukokotwa na wanyama kazi 23,631 na majembe ya mkono 2,650,000 yaliingizwa nchini. Aidha, Matrekta madogo ya mkono 170 yaliyoingizwa nchini mwaka wa 2001 chini ya msaada wa Serikali ya Japan yalisambazwa mikoani. Utaratibu wa kuwakopesha wakulima matrekta hayo madogo umeandaliwa na kutumwa mikoani. Chini ya utaratibu huo, mkulima atatakiwa kulipa nusu ya bei ya trekta na salio litakalobaki litalipwa katika kipindi cha miaka miwili chini ya udhamini wa Halmashauri ya Wilaya inayohusika. Mafundi sanifu 105 na wakulima 7,090 walipata mafunzo ya matumizi ya matrekta madogo ya mkono. Aidha, mabwana shamba 110 kutoka mikoa ya Arusha, Mbeya, Iringa, Ruvuma, Rukwa, Tabora, Mwanza na Shinyanga walipata mafunzo juu ya matumizi ya zana bora zinazokokotwa na wanyama na zinazowezesha uhifadhi wa udongo na unyevunyevu katika udongo.

## Uzalishaji, Uagizaji na Usambazaji wa Mbegu Bora

**44.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002 makadirio ya mahitaji ya mbegu bora yalikuwa ni tani 30,000. Upatikanaji wa mbegu bora ulifikia tani 12,025 kwa mazao ya nafaka, mikunde na mbegu za mafuta. Hili ni ongezeko la asilimia 47 ikilinganishwa na msimu wa 2000/2001 ambapo tani 8,196 zilipatikana. Mashamba ya mbegu ya Serikali yalichangia tani 594, sawa na asilimia 4, zikiwa ni mbegu za msingi. Chini ya utaratibu wa uzalishaji wa mbegu kwa kutumia wakulima wadogo, tani 553 zilizalishwa. Makampuni ya mbegu yaliingiza nchini tani 10,878 za mbegu.

## Wakala wa Mbegu

**45.** Kutokana na kufilisika kwa Kampuni ya Mbegu Tanzania (TANSEED), mfumo wa uzalishaji na usambazaji wa mbegu nchini ulisambaratika. Ili kujenga upya mfumo huo, wizara imeandaa mapendekezo ya kuanzisha wakala wa mbegu ambao utasimamia uzalishaji na usambazaji wa mbegu nchini. Aidha, waingizaji wa mbegu nchini watashauriwa kuzalisha mbegu hapa nchini. Uingizaji wa mbegu nchini utatakiwa ufuate utaratibu uliopo wa kisheria.

## Mfuko wa Pembejeo

**46.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo haukutoa mikopo kutokana na Serikali kusitisha utoaji wa mikopo hadi hapo utaratibu mzuri wa kutoa mikopo hiyo utakapobuniwa na kuidhinishwa na serikali. Hadi mwaka wa 2001, Mfuko ulikuwa umetoa mikopo 259 kwa wakopaji 211. Jumla ya shilingi bilioni 5,777,820,700 zilikopeshwa kwa watu binafsi na Vyama Vikuu vya Ushirika. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 2.25 zilikuwa zimerejeshwa kufikia mwezi wa Mei, 2002. Mfuko umechukua hatua za kuwafikisha mahakamani wadaiwa wake sugu 171 ambapo kesi

58 zilikuwa zimehukumiwa. Mahakama iliamuru mali za washitakiwa 35 ambazo waliweka rehani ziuzwe. Washitakiwa wengine 23 waliamriwa kulipa madeni yao kwa muda maalum wa kati ya mwezi mmoja hadi miezi sita na kwamba wakishindwa kufanya hivyo, mfuko utaomba Mahakama itoe kibali cha kuuza mali walizoweka rehani.

### Utafiti wa Mazao

**47.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002 shughuli za utafiti wa mazao ya kilimo ziliendelea kutekelezwa katika vituo vyote 17 vya utafiti. Tafiti zinazoendeshwa zilihusu maeneo makuu manne yafuatayo:-

- Uzalishaji wa mbegu bora,
- Mbinu bora za kilimo,
- Uchunguzi wa udongo, na
- Mbinu za udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao.

Shughuli hizi zilifanywa na vituo vya utafiti chini ya mradi wa Utafiti wa Kilimo, (*Tanzania Agricultural Research Project-TARP II*) kwa mkopo wa shilingi bilioni 3.5 kutoka Benki ya Dunia pamoja na fedha kutoka Hazina shilingi milioni 250. Watafiti waliendelea kufanya uchambuzi wa matatizo ya wakulima kwa kutumia mbinu shirikishi**. Katika mwaka wa 2001/2002 mbegu mama aina 19 zilizozalishwa na kutolewa na watafiti ni kama** zinavyoonyeshwa katika *Kiambatanisho Na.4.*

**48.** Mafanikio mengine yaliyopatikana kwenye utafiti ni pamoja na:

- Kituo cha Utafiti cha Mlingano kilikamilisha uchoraji wa ramani za mifumo ya kilimo kwa Kanda nne za Ziwa, Nyanda za Juu Kusini, Mashariki na Kaskazini. Kituo pia kiliendelea na utafiti wa matumizi ya mazao ya jamii ya mikunde katika kurutubisha ardhi.
- Kituo cha Naliendele kiliendelea kuboresha teknolojia za udhibiti wa magonjwa na wadudu wa zao la korosho. Miche 70,000 ya aina bora za mbegu za korosho zilizalishwa na kusambazwa katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Tanga.
- Kituo cha Maruku kilifanya majaribio ya aina bora nne za mbegu za migomba katika mashamba ya wakulima mkoani Kagera. Mbinu za udhibiti wa ugonjwa wa zao la kahawa (*Coffee wilt*) zilianzishwa kwa kushirikiana na *Tanzania Coffee Research Institute* - TACRI na Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Visumbufu vya Mimea (*Centre for Agricultural Bioscience International – CABI*). Aidha, miche zaidi ya 200,000 ya kahawa ya robusta iliyozalishwa kwa vikonyo (*Clonal coffee*) iliuzwa kwa wakulima mkoani Kagera.
- Kituo cha Dakawa kiliendelea kukamilisha taratibu za kutoa mbegu bora ya mpunga aina ya *SARO306* yenye uwezo wa kutoa tani 8 kwa hekta badala ya tani 3 kwa hekta na yenye ladha nzuri. Mbegu hii inatarajiwa kuidhinishwa kwa upandaji nchini mwaka wa 2002/2003.
- Vituo vya Ukiriguru na Ilonga, kwa kushirikiana na Bodi ya Pamba, viliendelea kuzalisha mbegu mpya za *UK91* na *ALA190* kwa kilimo cha mikataba. Mbegu ya *UK91* itaanza kulimwa katika eneo lote la Kanda ya Magharibi katika msimu wa 2003/2004.
- Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani ulianza katika vituo vya Uyole na Mlingano. Aidha, usanifu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani katika vituo vya Selian, Ilonga na Ukiriguru ulianza.
- Maabara za "*Biotechnology"* za Mikocheni na Tengeru ziliimarishwa na matayarisho ya ujenzi wa maabara nyingine Uyole yalianza.
- Katika kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora mpya kwa wakulima, vituo viliongeza juhudi za uzalishaji wa mbegu mama, mbegu za msingi na zilizothibitishwa katika mashamba ya vituo na

pia katika mashamba ya wakulima. Katika mwaka wa 2001/2002, hekta 1,353 zilipandwa mbegu katika vituo vya utafiti na kwenye mashamba ya wakulima ni kama ifuatavyo: **Ilonga hekta 213, Uyole hekta 212, Ukiriguru hekta 887, Selian hekta 25 na Ifakara hekta 16.**

**49.** Mheshimiwa Spika, mikutano ya kuhamasisha wadau kuchangia gharama za utafiti ilifanyika katika Kanda zilizokuwa zimebaki za Magharibi, Nyanda za Juu Kusini, Mashariki na Kaskazini. Halmashauri zote za Wilaya na Miji zilikubali kuchangia shilingi milioni moja hadi milioni tano kwa mwaka kwa kuzingatia mapato yao. Kanda ziliteua kamati maalum zinazosimamiwa na Wakuu wa Mikoa kwa ajili ya kuhamasisha uchangiaji katika mifuko ya utafiti ya kanda. Benki ya Dunia imekubali kuchangia kiasi kinacholingana na michango ya wadau. Hadi sasa uchangiaji ni kama ifuatavyo:-

- Kanda ya Kati Shs. 380,000,000.00
- Kanda ya Kaskazini Shs. 46,000,000.00
- Kanda ya Kusini Shs. 56,000,000.00

**50.** Uchangiaji wa mifuko ya kanda nne zilizobaki utaanza katika msimu wa 2002/2003. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Viongozi wote wa ngazi ya wilaya kwa juhudi zao zilizofanikisha zoezi hili.

## Taasisi za Utafiti wa Mazao ya Biashara

**51.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002, taasisi mpya za kusimamia utafiti wa baadhi ya mazao ya biashara zilianza **kufanya utafiti na kutoa huduma kwa wakulima kwa kuzingatia mahitaji yao**.

- Taasisi ya Utafiti wa Chai, *(Tea Research Institute of Tanzania – TRIT)*, iliendesha majaribio ya umwagiliaji maji mashambani na matumizi ya mbolea katika uzalishaji wa zao la chai. Aidha, taasisi ilianza kufufua mashamba ya chai ya wakulima wadogo wilayani Rungwe kwa kuwafundisha namna ya kukarabati mashamba na kueneza teknolojia bora za kilimo cha Chai.
- Taasisi ya Utafiti wa Kahawa, *(Tanzania Coffee Research Institute – TACRI),* iliendelea kubaini mbinu za udhibiti wa ugonjwa wa chulebuni *(CBD)* na kutu ya majani *(leaf rust)* ikiwa ni pamoja na kutathmini mbegu mpya zinazostahimili magonjwa hayo. Taasisi pia ilianzisha kitengo cha usambazaji wa teknolojia na mafunzo yanayolenga kuendeleza zao la kahawa.
- Taasisi ya Utafiti wa Tumbaku, *(Tobacco Research Institute of Tanzania – TORITA),* iliendesha majaribio ya matumizi ya mbolea na tathmini ya mbegu mpya ya tumbaku kwa kushirikiana na Kituo cha Utafiti cha Tumbi.

### MAZAO MBADALA

**52.** Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi uchumi wa Tanzania unategemea kuuzwa nje kwa mazao machache ambayo ni pamba, kahawa, korosho, chai, tumbaku, mkonge na pareto. Katika miaka ya karibuni, bei za mazao hayo kwenye soko la dunia zimeshuka sana kiasi cha kumfanya mkulima asiweze kuyazalisha kwa faida. Kushuka huko kwa bei za mazao yetu kwenye soko la dunia kunatokana na ushindani mkubwa unaosababishwa na nchi nyingi duniani kuzalisha mazao hayo kwa wingi. Wizara ya Kilimo na Chakula itaendelea kubuni mikakati ya kuwawezesha wakulima kuzalisha mazao hayo kwa bei nafuu na kwa ubora utakaoyawezesha kushindana katika soko la dunia. Pamoja na mikakati hiyo, inatubidi pia tuongeze idadi ya mazao ya biashara kwa kupanua kilimo cha mazao yasiyo ya asili *(non-traditional crops)* na mazao mbadala ambayo yana bei nzuri na ushindani mdogo katika soko la dunia kama njia ya kumwongezea mkulima kipato.

**53.** Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2001/2002, Wizara yangu iliendelea kuhudumia bustani sita za miti mizazi zilizoko Mpiji, Bagamoyo; Igurusi, Mbeya Vijijini; Kituo cha Utafiti wa Kilimo na Mafunzo *(Kilombero Agricultural Training and Research Institute - KATRIN),* Ifakara; Jegeto, Lushoto; Bugaga, Kasulu; na Songa, Muheza kwa lengo la kuhifadhi nasaba za mazao ya miti ya matunda na viungo. Nasaba za mazao hayo zimeanza kukusanywa kutoka mikoa ya Morogoro, Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Zanzibar na kupelekwa kwenye vituo vya Mpiji na *KATRIN* tayari kwa utafiti na uzalishaji kwa nia ya kusambazwa katika vituo vingine na kwa wakulima. Aina kumi za mazao ya viungo zimekusanywa ambazo ni tangawizi, bizari, vanila, pilipili, karafuu, vitunguu swaumu aina mbili, iliki aina mbili na mdalasini. Aidha, kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Wizara iliendelea kuhimiza kilimo bora cha mboga za majani, matunda, viungo na maharage ya mbegu pamoja na kuimarisha utafiti wa mazao haya katika kituo cha Tengeru kilichopo Arusha. Ili kuongeza upatikanaji wa mbegu bora za mboga za majani, wakulima katika mikoa ya Dodoma, Iringa na Morogoro waliwezeshwa kuzalisha mbegu hizo chini ya Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo (ASPS). Chini ya utaratibu huo, jumla ya kilo 1,147 za mbegu za nyanya, vitunguu, mchicha na bamia zilizalishwa.

## Mafunzo ya Kilimo kwa Wataalam na Wakulima

**54.** Mheshimiwa Spika, Wizara inaboresha mfumo mzima wa mafunzo kwa lengo la kuwapatia wahitimu elimu itakayowawezesha kuwashauri wakulima juu ya kilimo cha kibiashara. Wahitimu pia wataitumia elimu watakayopata kuwawezesha kujiajiri kwenye kilimo cha biashara. Mitaala miwili ya mafunzo ya mazao (*Crop Production and General Agriculture Production*) imeboreshwa kwa kuingiza masomo ya kilimo cha kibiashara (*agribusiness*), kilimo cha maksai, usindikaji wa mazao, hifadhi ya mazingira na elimu ya UKIMWI.

Mafunzo hayo yalitolewa kama ifuatavyo:-

***( i) Mafunzo kwa W ataalam W apya***

Katika mwaka wa 2001/2002, vyuo vya kilimo vilikuwa na wanafunzi 548, wanawake 122 na wanaume 426; idadi hii ni ongezeko la asilimia 26 ikilinganishwa na ile ya mwaka wa 2000/2001 ambapo kulikuwa na wanafunzi 435. Serikali ilifadhili karibu asilimia 85 ya wanafunzi wote.

***( ii) Mafunzo ya rejea kwa Maafisa Ugani***

Mwaka wa 2001/2002 Wizara iliandaa mitaala mitatu ya mafunzo ya rejea kwa maafisa ugani kwa mazao ya kahawa, pamba na korosho. Katika kipindi hicho, maafisa ugani 40 walipata mafunzo ya rejea kwenye zao la pamba ambayo yalitolewa na Chuo cha Kilimo cha Ukiriguru. Pia wataalam 40 wa ugani walipata mafunzo hayo kwenye zao la korosho yaliyotolewa na Chuo cha Kilimo cha Mtwara.

***( iii) Mafunzo kwa wakulima***

Katika kipindi cha 2001/2002 jumla ya wakulima 3,803 walipata mafunzo katika vyuo vya Uyole, Ukiriguru, Mtwara, Ilonga, Mlingano, *Kilimanjaro Agricultural Training Centre* (KATC), Moshi na Igurusi, Mbeya kuhusu kanuni za kilimo bora, kilimo cha maksai, usindikaji wa mazao, hifadhi ya mazingira na elimu ya UKIMWI. Ongezeko la idadi ya wakulima na wanafunzi waliohudhuria mafunzo hayo lilitokana na serikali kuyagharamia na jitihada za vyuo za kujitangaza **na kutoa mafunzo yanayotakiwa na walengwa.**

***( iv) Mafunzo ya wataalam wa kilimo nje ya nchi***

Katika mwaka wa 2001/2002 watumishi 201 walipata mafunzo nje ya nchi kwa kugharimiwa na miradi mbalimbali. Kati yao, 50 ni wanawake na 151 ni wanaume.

### *( v) Utayarishaji wa vitabu*

Chini ya Programu ya Kuisadia Sekta ya Kilimo (ASPS), Wizara imeandika vitabu vinne vya kiada juu ya matumizi bora ya maliasili, Kilimo cha biashara, Utunzaji na Uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa na Uzalishaji mbegu. Aidha, vitabu vinne vya rejea vimeandikwa kuhusu Magonjwa na afya za wanyama, Udhibiti wa magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea, Matumizi bora ya maji ya umwagiliaji Maji Mashambani na Sifa za mbegu za mazao.

## Hifadhi na Usalama wa Chakula

**55.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002, Wizara iliendelea kuratibu hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula na kutayarisha na kusambaza taarifa za uhakika wa chakula ndani na nje ya nchi. Tathmini ya hali ya chakula katika ngazi za Taifa, mikoa na wilaya zote imefanywa kupitia vijiji 3,064 vya sampuli pamoja na vituo 400 vya kuratibu hali ya hewa vilivyoko sehemu mbalimbali nchini. Ili kutunza vizuri takwimu na taarifa za chakula, Wizara yangu imeandaa mfumo wa kuingiza takwimu hizo kwenye kompyuta. Katika kazi hii, Wizara inashirikiana na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

**56.** Katika mwaka wa 2001/2002, Hifadhi ya Chakula ya Taifa ilipanga kununua tani 20,000 za mahindi, lakini ilifanikiwa kununua tani 18,971 tu, ambazo ni asilimia 95 ya lengo. Lengo la ununuzi halikufikiwa kwa sababu fedha zilipatikana baada ya msimu wa ununuzi kupita. Kiasi cha mahindi kilichonunuliwa kiliongeza akiba iliyokuwepo ya tani 46,300 kufikia tani 65,271. Mauzo kwa wananchi waliopungukiwa chakula yalifikia tani 600, wakati tani 8,000 ziliuzwa kwa taasisi mbalimbali za Serikali kwa mfano Idara ya Magereza, hospitali na shule. Aidha, Serikali imetoa tani 4,000 za mahindi kama msaada wa chakula kwa nchi za Malawi na Zambia, tani 2,000 kila mmoja.

## Usindikaji wa Mazao

**57.** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuanzisha na kuendeleza usindikaji wa mazao ya chakula, Wizara ya Kilimo na Chakula inashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha na kuendeleza viwanda vya kusindika mazao ili kuongeza ubora wa mazao hayo. Katika mwaka wa 2001/2002 mashine za kusindika matunda zilizoingizwa nchini zilikuwa 418 na mashine za kusaga mazao ya nafaka zilikuwa 4,680. Wizara inashirikiana na shirika la Nyumbu lililoko mkoa wa Pwani ili kuwezesha vikundi vya wakulima kupata mashine za bei nafuu za kusindika mazao yao. Ukarabati wa viwanda vya kusindika chai vilivyoko Katumba, Mwakaleli na Mponde na viwanda vya kuzalishaji sukari vya Kilombero, Mtibwa, TPC na Kagera uliendelea baada ya kubinafsishwa kwa lengo la kuongeza uzalishaji.

## Ubinafsishaji wa Mashirika ya Kilimo

**58.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002 mashirika yaliyobinafsishwa ni Makao Makuu ya Shirika la Usagishaji la Taifa (NMC) na Kampuni ya Sukari ya Kagera. Aidha, utaratibu wa kubinafsisha mashamba ya ngano ya NAFCO ulikamilika. Chini ya utaratibu huo, mashamba ya ngano ya Hanang yatabinafsishwa bila kugawanywa katika vijishamba vidogo vidogo. Mashamba ya mpunga yatabinafsishwa kwa kugawanywa katika maeneo madogo yanayoweza kuendeshwa kibiashara na wananchi. Hata hivyo miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani, vinu vya kukoboa mpunga na mitambo mikubwa itabinafsishwa kwa wawekezaji wenye mitaji na ujuzi wa kuviendesha kwa ufanisi. Ubinafsishaji wa Kiwanda cha chai cha Lupembe pamoja na shamba la Mlangali umekwamishwa na kesi iliyoko katika Mahakama ya Biashara kati ya Serikali na kampuni iliyokodisha kiwanda hicho inayoitwa *Dhow Merchantile Ltd.* Kazi ya kufuatilia mashirika na mashamba yaliyokwisha kubinafsishwa iliendelea kwa lengo la kujua maendeleo yake baada ya kubinafsishwa.

## Mafanikio ya Ubinafsishaji

**59.** Katika mwaka wa 2001/2002 uzalishaji wa sukari ulifikia tani 164,000 ikilinganishwa na tani 113,622 zilizozalishwa mwaka 1998/1999 kabla ya ubinafsishaji. Katika kipindi cha 2000/2001, uzalishaji wa chai ulikuwa tani 26,385 ikilinganishwa na tani 21,880 zilizozalishwa mwaka wa 1998/1999 kabla ya ubinafsishaji. Aidha, uzalishaji wa zao la mkonge uliongezeka na kufikia tani 23,540, sawa na ongezeko la asilimia 15 ikilinganishwa na tani 20,500 za mwaka wa 2000/2001. Inatarajiwa pia kuwa uzalishaji wa mpunga na ngano utaongezeka baada ya ubinafsishaji wa mashamba ya NAFCO kukamilika.

### MAENDELEO YA WATUMISHI

**60.** Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na kero ya watumishi kutopandishwa vyeo kwa muda mrefu, katika mwaka wa 2001/2002, Wizara iliweka utaratibu wa kupata takwimu na taarifa za utendaji kazi za watumishi za kila mwaka kutoka kwenye Halmashauri zote za Wilaya na Miji na kutoka kwenye taasisi zilizo chini ya Wizara. Utaratibu huo umeiwezesha Wizara kupandisha vyeo watumishi kwa mserereko mkubwa kuliko ilivyowahi kutokea miaka iliyopita. Watumishi wamepandishwa vyeo viwili kama ifuatavyo:-

| **WATUMISHI** | **IDADI** |
|---|---|
| Waliostahili Kupandishwa Vyeo | 6,865 |
| Waliopandishwa Vyeo hadi Juni, 2001 | 1,528 |
| Waliopandishwa vyeo mwezi wa Septemba, 2001 | 3,256 |
| Waliopandishwa vyeo mwezi wa Aprili, 2001 | 1,040 |
| **Jumla ya waliopandishwa vyeo** | **5,824** |
| **Ambao hawakupandishwa vyeo** | **1,041** |

Watumishi 1,041 ambao hawakupandishwa vyeo kwa mwaka wa 2001 watapandishwa vyeo katika mwaka wa 2002/2003. Watumishi wote 6,865 watapandishwa tena vyeo viwili viwili katika mwaka wa 2002/2003. Aidha, watumishi waliojiendeleza kimasomo na kupata sifa mpya na ambao walikuwa hawajarekebishiwa mishahara yao, walirekebishiwa mishahara ipasavyo. **Serikali za Mitaa na taasisi zilizo chini ya wizara ambazo hazijawarekebishia mishahara wataalam wa kilimo waliopandishwa vyeo, zinaagizwa kufanya hivyo mara moja.**

### MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA 2001/2002

## Fedha Zilizoidhinishwa na Kutolewa

**61.** Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2001/2002, Wizara ya Kilimo na Chakula **ilitengewa** shilingi bilioni 25.313 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 9.356 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 15.957 zilikuwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, shilingi bilioni 1.421 zilikuwa fedha za hapa na shilingi bilioni 14.536 zilikuwa fedha za kigeni. Mheshimiwa Spika, **kwa mara ya kwanza katika miaka kadhaa, Wizara ilipewa asilimia 90.7 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge.**

## MATUMIZI

**62.** Hadi tarehe 30 Juni, 2002 matumizi ya fedha yalikuwa kama ifuatavyo:

- Shilingi bilioni 8.484 fedha za matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 90.7 ya fedha zilizotengwa zilikuwa zimetumika.

- Shilingi bilioni 13.136 fedha za kigeni, sawa na asilimia 90 ya fedha za kigeni zilizotengwa, zilikuwa zimetumika.
- Shilingi bilioni 1.171 fedha za hapa sawa na asilimia 82.4 ya fedha za hapa zilizotengwa, zilikuwa zimetumia. *(Kiambatanisho Na. 5)*

### Mfuko wa Pembejeo

- Shilingi 456,730,000 zilizotengwa na kutolewa kwa ajili ya Mfuko wa Pembejeo, sawa na asilimia 5 ya fedha za hapa zilizotengwa, hazikutumika kutokana na matumizi ya fedha za mfuko kusitishwa. Maandalizi ya utaratibu wa kukopesha fedha za Mfuko yalikamilika na utaanza kutumika katika mwaka wa 2002/2003.

## IV. KAZI ZITAKAZOFANYIKA NA MATARAJIO KATIKA MWAKA WA 2002/2003

### Utekelezaji wa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo

**63.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003 Wizara itaendelea na juhudi zake za kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayofanya kilimo kisikue kwa kasi ya kuridhisha. Huu ni mwaka wa kwanza wa kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(The Agricultural Sector Development Strategy)*, ukiwa ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini. Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo umeandaliwa sambamba na Mkakati wa Maendeleo Vijijini. Aidha, Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa kushirikiana na Wizara za Ushirika na Masoko, Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imekamilisha matayarisho ya programu za kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Programu za kuendeleza sekta ya kilimo zilizoandaliwa zinaainisha nyanja kuu mbili ambazo ni **kukuza kilimo chenye tija na kukibadili kutoka kilimo cha kujikimu na kuwa cha kibiashara.**

**64.** Katika bajeti ya mwaka wa 2002/2003, Wizara imetenga shilingi 20,879,651,260, sawa na asilimia 70.4 ya bajeti yake, kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa programu za Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo. **Fedha hizi zitaelekezwa katika maeneo yanayomnufaisha mkulima moja kwa moja na katika mambo yenye uwezekano wa kutoa mafanikio katika kipindi kifupi. Programu za Kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Kilimo zitatekelezwa katika ngazi ya Wilaya. Kwa sababu hiyo, wilaya zinatakiwa kuandaa programu zao za kuendeleza kilimo na kuzikamilisha kabla ya mwezi wa Oktoba, 2002 ili ziunganishwe kwenye bajeti zao za mwaka wa 2003.**

**65.** Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka wa 2002/2003 **imeongezwa** kwa asilimia 32 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa 2001/2002, lakini iko chini kuliko bajeti ya mwaka wa 1998/1999 kwa shilingi 3,904,378,700. Kilichotokea kuanzia miaka ya themanini ni kushuka kwa uwekezaji katika kilimo mwaka hadi mwaka mpaka kufikia kiwango cha chini kabisa mwaka wa 2001/2002.

**66.** Mheshimiwa Spika, moja kati ya matatizo makubwa yanayokwamisha kukua kwa kilimo ni kushuka sana kwa uwekezaji katika kilimo na kutokuwapo kwa utaratibu wa kumwezesha mkulima kupata mikopo ya kununulia mahitaji yake ya kilimo. Fedha zilizotengwa katika bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula mwaka huu zitasaidia kupunguza tatizo hili. Hata hivyo, mahitaji ya fedha ni makubwa na Serikali peke yake haitamudu kutosheleza mahitaji hayo. Wizara ya Fedha imekubali kupanua ule utaratibu aliotangaza Waziri wa Fedha wakati wa Hotuba yake ya Bajeti ya Mwaka wa 2002/2003, wa kutoa dhamana kwa mabenki ili kuyawezesha kutoa mikopo kwa ajili ya mauzo ya bidhaa nchi za nje, ili ujumuishe mikopo kwa sekta ya kilimo. **Chini ya utaratibu huu, Serikali kupitia mabenki, itatoa dhamana kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kilimo.**

Kwa mujibu wa maelekezo ya Waziri wa Fedha, Mfuko wa Kudhamini Mikopo kwa Mauzo ya bidhaa Nje ya nchi utadhamini uzalishaji wa mazao ya biashara, uagizaji na utengenezaji wa zana na pembejeo za kilimo kama vile mbolea, madawa ya kilimo na majembe ya kukokotwa na wanyama. Aidha, Mfuko huo, utadhamini ununuzi wa mazao ya biashara na usindikaji wa mazao ya kilimo kwa ajili ya masoko ya ndani na nje ya nchi. Wizara, kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Kilimo, itaweka utaratibu na masharti ya kutumia huduma hii ili wakulima, wafanyabiashara na wawekezaji waweze kukopa na kuwekeza katika kilimo.

**67.** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Wizara za Fedha, Ushirika na Masoko, Maji na Mifugo na Benki Kuu ya Tanzania inaandaa mapendekezo ya mpango wa kugharamia kilimo ambao utapendekeza njia mbalimbali za kupata fedha kwa ajili hiyo na wajibu wa wadau wote katika suala hili. Ni mapema mno kusema utaratibu huo utakuwaje, lakini inatarajiwa kwamba utawezesha kuwepo kwa taasisi ya fedha ambayo itaanzishwa na Serikali ambayo itaunganisha mifuko na michango mbalimbali iliyopo na michango na akiba za wadau na ambayo baadaye itamilikishwa kwa wakulima wenyewe. Aidha, Wizara ya Fedha imeagiza wadau wote wa kilimo waunganishe nguvu kukamilisha maandalizi ya utaratibu huo. Kama sehemu ya mkakati huo, akiba za wananchi zitawekewa utaratibu utakaowezesha zikopeshwe kwa ajili ya uwekezaji katika kilimo.

**68.** Katika miaka ya hivi karibuni, kumeanzishwa vyama vya kuweka na kukopa ambavyo vinajulikana kwa majina mbalimbali kwa mfano, SACCOS, Benki za Wananchi, Benki Kata na kadhalika. Vyama hivyo vimekuwa na mafanikio makubwa sana katika kukusanya akiba za wanachama na katika kutoa mikopo kwa wanachama. Benki ya CRDB na washirika wao, imeanzisha utaratibu wa kusaidia baadhi ya taasisi hizi ambao umekuwa na mafanikio makubwa sana. Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza sana Benki ya CRDB kwa kazi nzuri wanayofanya. Yote haya yataunganishwa na kuzingatiwa katika utaratibu wa kugharamia kilimo unaoandaliwa.

**69.** Katika nchi zote duniani, ukiondoa Tanzania, akiba za wananchi zinazohifadhiwa katika mabenki hukopeshwa kwenye shughuli za kiuchumi na ndizo zinazowezesha kukua kwa uchumi. Inatubidi na sisi tujenge utamaduni wa kukopa kutoka kwenye mabenki yetu na kulipa madeni kwa mujibu wa masharti ya mikopo hiyo. Kuna mifano mingi nchini ya ukopeshaji uliofanyika kwa mafanikio na Watanzania sio tofauti na wanadamu wengine katika suala hili.

**70.** Kukamilika kwa utaratibu wa kugharamia kilimo kutawezesha kutekelezwa kwa ukamilifu zaidi kwa Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa 2000 ya Chama Cha Mapinduzi na Mwelekeo wa Sera za CCM hadi 2010, hususan kuhusiana na uwezeshaji na kupunguza umaskini. Ujuzi na uzoefu tulionao kama Taifa na rasilimali tulizo nazo za watu, ardhi kubwa, maji na hali nzuri ya hewa vikiunganishwa na mipango mizuri ya kuwekeza katika kilimo vinanipa matumaini kwamba siku inakaribia kilimo chetu kitaonyesha mafanikio yanayokusudiwa.

**71.** Malengo makuu ya kilimo katika mwaka wa 2002/2003, kama yalivyoorodheshwa katika Mkakati wa Maendeleo ya Kilimo, yatakuwa kama ifuatavyo: -

- Kilimo kukua kutoka asilimia 5.5 ya 2001/2002 hadi asilimia 6.0 ifikapo mwaka wa 2003 na kuendelea kukua kuelekea kwenye asilimia zaidi ya kumi ili kukiwezesha kuongeza mchango wake katika pato la taifa na katika kupunguza umaskini.
- Kufanya kilimo kiwe cha kisasa, cha kibiashara na chenye tija.
- Kuongeza usalama na uhakika wa chakula kuanzia ngazi ya kaya hadi Taifa.
- Kuongeza wingi na ubora wa mazao yanayouzwa nje ya nchi ili kuongeza mapato ya fedha za kigeni za Taifa.

**72.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003 Wizara ya Kilimo na Chakula imetengewa jumla ya shilingi **14,658,874,900** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **18,603,608,100** kwa shughuli za maendeleo. Wizara itaelekeza fedha hizi kutekeleza majukumu muhimu yafuatayo: -

- **Kutekeleza Programu za Mkakati wa Kilimo** na kutathmini matokeo na michango ya programu hizo katika ukuaji wa sekta ya kilimo, pato la Taifa, mapato ya fedha za kigeni, upatikanaji wa chakula nchini na upunguzaji wa umaskini. Wilaya nazo zinatakiwa kuandaa programu zao za kuendeleza kilimo na kuzikamilisha kabla ya mwezi Oktoba, 2002 ili ziunganishwe kwenye bajeti zao za mwaka wa 2003.

  **Chini ya utekelezaji wa programu hizo**, mambo yafuatayo yanayotarajiwa kutupa matokeo ya haraka, yatafanyika kwa kutumia fedha za Serikali kama ifuatavyo:-

  - Kuzalisha kwa wingi (seed multiplication) aina 15 za mbegu zilizotafitiwa na Vituo vya Utafiti, kwa ngazi ya mbegu mama na ngazi ya mbegu za msingi. Aina hizi za mbegu zinajumuisha aina tano za mbegu za mahindi, aina mbili za mbegu za mpunga, aina sita za mbegu za mikunde na aina mbili za mbegu za mafuta. Kazi hii imetengewa **shilingi milioni 211.4**.
  - Kukarabati skimu nane ndogo ndogo za umwagiliaji maji mashambani zilizojengwa miaka iliyopita ambazo hazifanyi kazi kutokana na matatizo mbalimbali. Kazi hizi zimetengewa **shilingi milioni 500**.
  - Mfuko wa pembejeo utaanza tena kukopesha pembejeo na zana za kilimo kwa kupitia kwenye mabenki, vyama vya kuweka na kukopa na vyama vya ushirika. Katika mwaka wa 2002/2003 Mfuko utakuwa na jumla ya **shilingi bilioni 3.2** zikiwemo **shilingi bilioni 2.5** kutoka kwenye bajeti ya mwaka huu na **shilingi milioni 456.7** ambazo hazikukopeshwa mwaka wa 2001/2002 na albaki ya **shilingi milioni 300** iliyokuwapo kwenye Mfuko.
  - Kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao. Kazi hii imetengewa **shilingi bilioni 1.4** kwa ajili ya shughuli za udhibiti na kwa ajili ya malipo ya ada kwa Mashirika ya Kimataifa tunayoshirikiana nayo kudhibiti nzige na kwelea kwelea.
  - Kuendeleza kilimo cha wanyama kazi na kufufua vituo vya maksai. Kazi hizi zimetengewa **shilingi milioni 300**.
  - Hifadhi ya Taifa ya Chakula ambayo imetengewa **shilingi bilioni 1.9** kwa ajili ya kununulia mahindi tani 16,400 na kuifanya iwe na jumla ya tani 67,900.
  - Kuandaa mwongozo wa kuziwezesha wilaya kuandaa mikakati na programu zao za kundeleza kilimo. Kazi hii imetengewa **shilingi milioni 9.2**.

Miradi karibu yote iliyoko kwenye Wizara inatatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na wahisani. Kazi zifuatazo zitatekelezwa chini ya miradi mitano iliyopo.

- **Kuendeleza utafiti wa teknolojia bora za kilimo**. Lengo la utafiti huu ni kumwezesha mkulima kupunguza gharama za uzalishaji, kumwongezea mavuno na tija na hivyo kumpunguzia umaskini.
- **Kukarabati na kujenga miundombinu katika vituo vya utafiti na mafunzo.** Ukarabati utahusu maabara, ofisi na mabweni kwenye vituo vya utafiti na Vyuo vya mafunzo. Miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani itajengwa kwenye Vituo vya utafiti vya Uyole, Mlingano na Ilonga.
- Kueneza na kuendeleza matumizi ya **Mbinu Shirikishi Jamii** na **Shamba Darasa** nchi nzima. Warsha zitaandaliwa kuwafundisha viongozi katika ngazi za wilaya na mikoa mbinu hizo pamoja na mbinu za udhibiti husishi.
- M**itaala mitano ya mafunzo ya maafisa Ugani** itarekebishwa ili kuingiza vipengele muhimu vya kilimo cha biashara, hifadhi ya mazingira na elimu ya UKIMWI. Lengo kuu ni kuwapatia wahitimu elimu itakayowawezesha kuwashauri wakulima juu ya kanuni bora za kilimo cha biashara na pia kuwawezesha kujiajiri wenyewe kwenye shughuli za kilimo.

- **Kueneza teknolojia rahisi za kilimo cha umwagiliaji maji mashambani** na kuhamasisha wakulima kuunda vikundi vya ushirika wa wamwagiliaji maji mashambani. Teknolojia zitakazoenezwa ni pamoja na mbinu za uvunaji maji na uchimbaji wa visima vifupi.
- **Kuandika vitabu vya aina tano vya kiada na rejea** kuhusu kanuni bora za kilimo kwa ajili ya Vyuo vya Kilimo, Wakulima na Maafisa Ugani. Vitabu hivyo vitatumika kuwapatia wakulima elimu ya kilimo katika mazingira yao.
- **Kupunguza upotevu wa mavuno** kwa kuwafundisha wakulima na maafisa ugani, teknolojia rahisi zinazoweza kutumika katika kuhifadhi mazao.

**Mazao ya Biashara**

**73.** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula, itaendelea kusimamia na kuendeleza uzalishaji wa mazao makuu ya biashara ambayo ni pamba, tumbaku, pareto, kahawa, korosho, sukari, mkonge na chai. Uendelezaji wa uzalishaji wa mazao hayo, utafanywa kwa kuzingatia mikakati iliyoandaliwa na Bodi za mazao. Mikakati hiyo, pamoja na mambo mengine, inalenga kuongeza uzalishaji wa mazao kwa kutoa mafunzo ya kilimo bora kwa wakulima, kupanua eneo la uzalishaji, kuhakikisha upatikanaji na matumizi sahihi ya pembejeo na zana za kilimo, kusimamia ubora wa mazao, hususan kuhakikisha kwamba ubora wa mazao unazingatiwa kwa kufuata madaraja yanayokubalika kitaifa na kimataifa, na kuhakikisha kwamba mazao yanasindikwa kabla ya kutafutiwa masoko ndani na nje ya nchi.

***Pamba***

**74.** Katika mwaka wa 2002/2003, uzalishaji wa pamba unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 149,091 za mwaka wa 2001/2002 hadi kufikia tani 175,500, sawa na ongezeko la asilimia 15. Taifa bado lina fursa kubwa ya kupanua eneo linalolimwa pamba, hususan katika Kanda ya Mashariki na Mikoa ya Singida na Kigoma. Bodi ya Pamba na Halmashauri za Wilaya zitaendelea kuhamasisha wakulima kupanua na kuendeleza kilimo bora cha pamba katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Kilimanjaro, Iringa, Arusha, Tanga, Singida na Kigoma. Katika Kanda ya Pamba ya Magharibi tani 555 za mbegu mpya ya pamba aina ya UK91 zitapandwa mwaka wa 2002/2003 na tani 10,000 za mbegu zinatarajiwa kuvunwa. Mahitaji ya mbegu ya pamba ya kanda hiyo katika msimu wa 2003/2004 ni tani 4,000. Hivyo, mbegu ya UK91 itaanza kulimwa katika eneo lote la Kanda ya Magharibi kuanzia msimu wa 2003/2004.

**75.** Katika kanda ya Pamba ya Mashariki, tani 38 za mbegu ya pamba aina ya IL85 zitapandwa katika mwaka wa 2002/2003 na tani 1,200 za mbegu ya pamba zinatarajiwa kuvunwa. Kwa kuwa mahitaji ya mbegu ya pamba Kanda ya Mashariki msimu wa 2003/2004 ni tani 4,000, mbegu ya pamba aina ya IL85 itaanza kulimwa katika eneo lote la Kanda ya Pamba ya Mashariki kuanzia msimu wa 2003/2004. Bodi ya Pamba itaendelea kusimamia ubora wa zao la pamba na maslahi ya mkulima.

**76.** Bodi ya Pamba, itakarabati viwanda vya kuchambua pamba vya Moshi na Same mkoani Kilimanjaro, katika Kanda ya Mashariki. Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya rejea na maelekezo kwa wataalam wa ugani walioko kwenye Halmashauri za Wilaya, kwa lengo la kuwapa ujuzi wa kusimamia na kufundisha wakulima kilimo bora cha pamba.

***T umbaku***

**77.** Uzalishaji wa Tumbaku katika mwaka wa 2002/2003 unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 31,700 za mwaka wa 2001/2002 hadi tani 45,450, sawa na ongezeko la asilimia 30. Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Bodi ya Tumbaku, itatoa mafunzo kwa wakulima 4,250 juu ya kanuni bora za kilimo cha tumbaku. Mafunzo hayo yatatolewa kupitia kwenye vyama vya msingi vya ushirika kumi na vitano mkoani Tabora na kumi mkoani Ruvuma. Mafunzo ya kilimo bora cha tumbaku yatatolewa kwa maafisa ugani 141 katika mikoa ya Ruvuma na Tabora. Kuanzia mwisho wa mwezi wa Julai, 2002, kipindi cha

redio cha ***Tumbaku ni Utajiri*** kitaanza tena kutangazwa na Redio Tanzania. Wizara itaandaa vikao maalum vya wadau wa zao la tumbaku, kuona wanavyoweza kuunganisha nguvu kuendeleza zao hili.

***Sukari***

**78.** Katika mwaka wa 2002/2003, uzalishaji wa sukari unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 163,994 zilizozalishwa mwaka wa 2001/2002 hadi tani 213,000, sawa na ongezeko la asilimia 29.5. Ongezeko hili litatokana na ongezeko la uzalishaji kwenye viwanda vya sukari vya Kilombero, Mtibwa, na TPC na kiwanda cha Kagera kuanza kuzalisha sukari katika nusu ya pili ya mwaka. Uzalishaji wa sukari kwenye viwanda hivyo ni kama ifuatavyo:

| **KIWANDA** | **2001/2002 (Tani)** | **2002/2003 (Tani)** | **% ONGEZEKO** |
|---|---|---|---|
| Kilombero | 72,498 | 95,000 | 31 |
| Mtibwa | 42,314 | 45,000 | 6.3 |
| TPC | 49,686 | 58,000 | 16.7 |
| Kagera | 0 | 15,000 | - |
| **JUMLA** | **163,994** | **213,000** | **29.5** |

Kiwanda cha Mtibwa kimeomba kuongezewa eneo kwa ajili ya kupanua shamba lao la miwa kukidhi mahitaji ya kiwanda kinachopanuliwa. Serikali inaangalia uwezekano wa kuwapatia eneo la nyongeza pamoja na eneo kwa ajili ya wakulima wadogo wa miwa.

Aidha, Wizara itashirikiana na mikoa kuweka mazingira mazuri zaidi ya uzalishaji kati ya viwanda vya sukari na wakulima wadogo. Bodi ya Sukari itaendelea kusimamia na kuratibu mpango wa kuendeleza wakulima wadogo wa miwa, hususan katika mabonde ya Mto Kilombero na Kagera. Lengo ni kuwa na wakulima wadogo wapatao 10,000 ifikapo mwaka wa 2003 watakaoshiriki katika mpango wa kilimo cha miwa cha mkataba na viwanda vya sukari. Mpango huo utakwenda sambamba na utoaji wa mafunzo ya kilimo bora cha miwa. Aidha, Bodi ya Sukari itaendelea kusimamia uendelezaji wa zao la miwa na uzalishaji na biashara ya sukari nchini kwa kutumia sheria mpya ya sukari iliyopitishwa na Bunge mwezi wa Novemba, 2001.

***Mkonge***

**79.** Uzalishaji wa mkonge katika mwaka wa 2002/2003, unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 23,542 za katani za mwaka wa 2001/2002 hadi kufikia tani 25,000, sawa na ongezeko la asilimia sita. Ongezeko hilo litatokana na mavuno ya tani 2,000 za katani kutoka kwenye hekta 2,000 zilizopandwa mwaka wa 1998. Aidha, ongezeko lingine litatokana na mashamba yaliyokarabatiwa. Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi ya Afrika (BADEA), imetoa msaada wa kiufundi wa dola za Kimarekani 370,000 kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha zao la mkonge kwa wakulima wadogo wa mikoa ya Mara, Mwanza na Shinyanga. Chini ya mpango huo, jumla ya hekta 10,000 za zao hilo zitastawishwa katika mikoa hiyo katika miaka mitano ijayo kuanzia msimu wa 2002/2003.

Sekta ya mkonge imeanza uchunguzi unaolenga kuongeza matumizi ya mmea wa mkonge. Kwa sasa ni asilimia tatu hadi nne tu ya mmea huu ndiyo inayotumika kuzalisha katani. Mkopo wa USD 5.7 milioni, kutoka "*Common Fund for Commodities* – CFC", kupita Shirika la UNIDO, unagharamia uchunguzi huo ili kupata matumizi mengine zaidi ya mkonge, kama uzalishaji wa nishati, karatasi, madawa, mbolea na pombe (*alcohol*).

***Chai***

**80.** Katika mwaka wa 2002/2003, uzalishaji wa chai unategemewa kuongezeka kutoka tani 26,848 zilizozalishwa mwaka wa 2001/2002 hadi tani 30,875 sawa na ongezeko la asilimia 15. Ongezeko hili linatarajiwa kufikiwa kutokana na ukarabati wa mashamba ya chai ya wakulima wadogo uliofanywa katika wilaya za Njombe, Korogwe, Rungwe na Bukoba. Aidha, wakulima wadogo watapatiwa mbolea na madawa. Mkazo utawekwa katika uzalishaji wa miche kwa ajili ya kupanda mashambani kujaza nafasi zilizo wazi. Huduma za ugani kwa ajili ya wakulima wadogo zitaimarishwa. Wizara ya Kilimo na Chakula na Bodi ya Chai zitaendelea kushughulikia migogoro iliyopo kuhusiana na baadhi ya mashamba na kuhakikisha kwamba mashamba hayo yanarudia kuzalisha kikamilifu na pia kuhakikisha kwamba wawekezaji katika viwanda vya kusindika chai, wanaviendeleza kufuatana na mikataba ya ubinafsishaji.

***Pareto***

**81.** Uzalishaji wa pareto unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 3,500 za mwaka wa 2001/2002 hadi tani 4,000 mwaka wa 2002/2003, sawa na ongezeko la asilimia 14. Bodi ya Pareto, itazalisha tani 15 za mbegu za pareto na kuzisambaza kwa wakulima katika mikoa ya Iringa, Ruvuma, Mbeya, Arusha na Kilimanjaro. Katika kukabiliana na tatizo la ukosefu wa soko, Bodi ya Pareto itaendelea kusajili makampuni binafsi yatakayonunua na kusindika pareto. Yapo makampuni kadhaa ambayo yameonyesha nia ya kuwekeza katika usindikaji wa zao hili, jambo ambalo litapunguza sana matatizo ya kuuza pareto.

***Kahawa***

**82.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2000/2001, uzalishaji wa kahawa ulishuka kutoka tani 58,134 hadi 36,175 zilizozalishwa mwaka wa 2001/2002. Katika mwaka wa 2002/2003 lengo litakuwa kuzalisha tani 54,000 za kahawa sawa na ongezeko la asilimia 49 ikilinganishwa na uzalishaji katika mwaka 2000/2001. Ongezeko hili litawezekana kutokana na kukarabati mashamba ya kahawa, kupanda upya mashamba ya zamani kwa miche ya kahawa inayostahimili ugonjwa wa chulebuni, ujenzi wa vinu vya kumenya kahawa *(central pulperies)* na ukarabati wa barabara za kahawa. Kazi hizo zitagharamiwa na Mfuko wa Stabex. Mkazo utawekwa katika kuongeza ubora wa kahawa yetu katika ngazi zote za uzalishaji na kuhimiza wanunuzi kutoa bei kwa kuzingatia ubora. Wakulima wa kahawa aina ya *robusta* watahamasishwa kukoboa kahawa yao kwa kutumia mashine za mikono (*hand pulperies*) kabla ya kuiuza.

**83.** Katika kukabiliana na magonjwa ya chulebuni (CBD) na kutu ya majani, aina nane mpya za kahawa ya *arabica* zinazohimili magonjwa hayo zimegunduliwa. Aina hizo mpya, zitazalishwa kwa wingi na kusambazwa kwa wakulima wa maeneo yanayolima kahawa aina ya *arabica*, hususan katika mikoa ya Mbeya, Arusha, Kilimanjaro, Ruvuma, Kigoma na Rukwa. Matumizi ya miche hiyo yanatarajiwa kupunguza gharama za uzalishaji na hivyo kuwawezesha wakulima kuendelea kulima zao la kahawa kwa faida. Aidha, katika kukabiliana na matatizo ya pembejeo kwa zao la kahawa, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko, itaendeleza utaratibu wa sasa wa Vocha sambamba na utaratibu mpya wa stakabadhi ya maghala *(Warehouse Receipt System)*, pamoja na mikopo ya pembejeo kutoka kwenye Mfuko wa Pembejeo.

***Korosho***

**84.** Uzalishaji wa korosho unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 67,369 zilizozalishwa mwaka wa 2001/2002 hadi kufikia tani 125,000 mwaka wa 2002/2003, sawa na kiasi kilichozalishwa mwaka wa 2000/2001. Ongezeko hili litatokana na kuwafikishia wakulima dawa ya kudhibiti ugonjwa wa *ubwiri unga* mapema, kuongeza uwezo wa kubangua korosho kutokana na ukarabati wa viwanda vya kubangua korosho vya Kibaha na Masasi, kuongezeka kwa mashine ndogo ndogo za kubangua korosho na kuongezeka kwa bei ya koshoro. Kutokana na ukarabati wa viwanda vya korosho vya Kibaha na Masasi, tutakuwa na

uwezo wa kubangua hadi tani 26,220 za korosho mwaka wa 2002/2003. Aidha, Wizara ya Kilimo na Chakula itaendelea kuhimiza matumizi ya mashine ndogo za kubangua korosho zinazotengenezwa na kiwanda cha Nyumbu kilichoko Kibaha.

### Mazao Mbadala

**85.** Mheshimiwa Spika, uchumi wa Tanzania unategemea kuuzwa nje kwa mazao machache ambayo ni pamba, kahawa, korosho, chai, tumbaku, mkonge na pareto. Katika miaka ya karibuni, bei za mazao hayo kwenye soko la dunia zimeshuka sana kiasi cha kumfanya mkulima asiweze kuyazalisha kwa faida. Kushuka huko kwa bei ya mazao yetu kwenye soko la dunia kunatokana na ushindani mkubwa unaosababishwa na nchi nyingi duniani kuzalisha mazao hayo kwa wingi. Wizara ya Kilimo na Chakula itaendelea kubuni mikakati ya kuwawezesha wakulima kuzalisha mazao hayo kwa gharama ndogo na kwa ubora utakaoyawezesha kushindana katika soko la dunia. Kushuka kwa bei ya mazao makuu ya biashara kunaathiri vibaya mapato ya Taifa ya fedha za kigeni, vita dhidi ya umaskini na kwa hiyo, uchumi na maendeleo ya nchi. Ili kuondokana na athari hizi, inatubidi tuongeze idadi ya mazao ya biashara yanayozalishwa kwa ajili ya kuuzwa nje ya nchi kwa kupanua sana kilimo cha mazao yasiyo ya asili (*non-traditional crops*) na mazao mbadala ambayo yana bei nzuri na ushindani mdogo katika soko la dunia.

**86.** Baadhi ya mazao hayo ni mbegu za mafuta (ufuta, alizeti na mlonge), viungo mbalimbali (iliki, vitunguu, vanilla na bizari), mikunde (dengu, kunde, maharage na choroko), maua na matunda. Ili kufanikisha lengo hili, Wizara ya Kilimo na Chakula, itaendelea kukusanya mazao ya viungo, kuyafanyia tathmini, kuchagua yenye nasaba bora kwa lengo la kuyaendeleza na kuyasambaza kwa wakulima. Aidha, wakulima katika skimu za umwagiliaji maji mashambani watahimizwa kupanda dengu baada ya kuvuna mpunga. Kilimo cha migomba kitatiliwa mkazo kwa ajili ya kuzalisha ndizi za kuuza nje ya nchi.

### Huduma za Utafiti wa Kilimo

**87.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara ya Kilimo na Chakula, itaendelea kufanya utafiti wa kilimo katika vituo vyake 17 kama ifuatavyo:

- Kufanya utafiti unaolenga mahitaji halisi ya walengwa,
- Kufanya utafiti utakaobuni mbinu za kuzalisha mazao kwa gharama nafuu na zitakazo ongeza tija
- Kufanya utafiti wa aina bora za mbegu za mazao zinazostahimili ukame, magonjwa, wadudu waharibifu na zenye uwezo wa kutoa mazao mengi kwa hekta,
- Kufanya utafiti wa udhibiti husishi wa kukabiliana na visumbufu vya mimea na mazao,
- Kufanya utafiti wa mbinu za kuzalisha mazao ambao utazingatia wingi na ubora wa zao husika,
- Kufanya utafiti wa kuchunguza udongo, kilimo mseto, utumiaji wa zana bora za kilimo na sayansi ya jamii katika sekta ya kilimo kwa kuzingatia masuala ya jinsia,
- Kufanya utafiti wa mazao yasiyo asilia ili kupata mazao mbadala ya biashara.

Mikakati itakayotumika katika tafiti hizi ni kuwashirikisha wakulima katika shughuli za utafiti na majaribio yatakayofanywa katika mazingira yao.

**88.** Katika mwaka wa 2002/2003, watafiti, kwa kushirikiana na wakulima, wataendelea kuibua teknolojia mpya, kwa lengo la kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa ufanisi na hivyo kuongeza tija na faida kama ifuatavyo:

- Kituo cha Selian kitaendelea na uzalishaji wa mbegu mpya za mahindi (*Lishe 1* na *Lishe M1*, *Situka M1* na *Situka 1*), kwa ngazi ya mbegu mama na msingi ili ziweze kufikishwa kwa wakulima

msimu wa 2003/2004. Mahindi aina ya *Lishe* yana sifa ya kuwa na viini-lishe vingi vya aina ya protein, hivyo kuwa na uwezo wa kupunguza utapiamlo yanapotumiwa kwa chakula. Mahindi aina ya *Situka* yana uwezo wa kustawi na kutoa mavuno ya tani 3 – 4 kwa hekta kwenye maeneo ya ukame na yenye rutuba hafifu. Aidha, kituo cha Uyole kitaendelea kuzalisha mbegu ya mahindi aina ya *UH615,* inayostahimili ugonjwa wa ukungu wa mahindi, kwa ngazi ya mbegu zilizothibitishwa na kuziuza kwa wakulima wa Kanda ya Nyanda za Juu kusini.

- Kituo cha Ukiriguru, kwa kushirikiana na Bodi ya Pamba, kitakamilisha uzalishaji wa mbegu ya pamba aina ya *UK91* kwa kutumia wakulima wa mkataba.
- Kituo cha Utafiti cha Ilonga, Morogoro kitashirikiana na Maafisa Ugani, wakulima na mashamba ya mbegu za msingi katika kuongeza uzalishaji wa aina za mbegu za kunde, pamba na mtama. Lengo likiwa ni kufupisha muda wa mbegu hizo bora kuwafikia wakulima.
- Kituo cha Mlingano kitaendelea kutekeleza majukumu ya kitaifa ya kutafiti udongo. Aidha, kituo hicho kitakamilisha kuandaa ramani za mifumo ya kilimo ya Kanda za Kati, Kusini na Magharibi. Ramani hizo zitaonyesha mazao yanayofaa kulimwa katika kanda na kila wilaya.
- Kituo cha KATRIN, Ifakara, kitaimarishwa ili kufanya utafiti wa mazao ya viungo *(spices)* na kuwa kitovu cha kutoa mbegu za viungo. Tayari aina kumi za mazao ya viungo, tangawizi, bizari, pilipili na mdalasini zimekusanywa ili kufanyiwa utafiti.
- Kituo cha Tumbi kitasambaza teknolojia ya kilimo cha mzunguko wa miti na mazao *(rotational woodlots)* vijijini. Vile vile, kituo hicho kitaendelea na utafiti wa matunda asili, ikiwa ni pamoja na uzalishaji kwa kutumia mbegu na vikonyo na usindikaji wa matunda asili. Kituo kitashirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Tumbaku (TORITA) kufanya utafiti wa zao la tumbaku, hususan katika kuchunguza ubora wa aina mpya ya mbegu za tumbaku.
- Kituo cha Naliendele, Mtwara, kitaendelea kutafiti mbinu bora za kuongeza uzalishaji wa korosho, ufuta, karanga pamoja na kudhibiti visumbufu vya mazao hayo. Aidha, kituo kitafanya utafiti wa matumizi ya ***mabibo*** kwa lengo la kumuongezea kipato mkulima.
- Kazi ya utafiti wa zao la kahawa, chai na tumbaku itafanywa na taasisi za wadau wa mazao hayo (TRIT, TACRI na TORITA).
- Ukarabati wa miundombinu katika vituo sita vya utafiti unaoendeshwa chini ya mradi wa TARP II utaendelea.

## Kuhimiza uzalishaji wa mazao kufuatana na Kanda za Kilimo (*Agro-ecological zones*)

**89.** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula itaendelea kuhimiza wakulima kupanda mazao kulingana na hali ya hewa na udongo katika maeneo yanayohusika. Tayari Wizara imekwishaainisha mazao yanayofaa kwa kila kanda (*Kiambatanisho Na. 6*). Aidha, Wizara itakamilisha maandalizi ya ramani za mazao yanayostawi katika kila wilaya. Kazi hiyo itatekelezwa na Kituo cha Utafiti cha Mlingano. Kwa maeneo yenye ukame, kipaumbele kitawekwa kwenye mazao yanayostahimili ukame kama vile muhogo, viazi vitamu, mtama na uwele. Serikali za Mitaa zinashauriwa kusimamia wakulima kupanda mazao yanayostawi kwenye maeneo yao na kutunga sheria ndogo za kuhakikisha utekelezaji.

### Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani

**90.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003 Wizara itaendelea kukarabati miundo mbinu ya skimu za umwagiliaji maji 14 zenye eneo la hekta 4,495 zilizojengwa zamani na kueneza teknolojia rahisi ya umwagiliaji katika miradi ya kilimo cha umwagiliaji maji mashambani *(Kiambatanisho Na. 7).* Aidha, wizara itawahamasisha wakulima kuchangia gharama za ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Kazi zitakazofanywa ni kama ifuatavyo:

### Ukarabati wa Skimu za Umwagiliaji Maji Mashambani Zilizochakaa

**91.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara ya Kilimo na Chakula, itakarabati skimu ambazo miundombinu yake imechakaa na kusimamia uanzishaji na uimarishaji wa Vyama vya Wamwagiliaji katika Miradi ambayo ujenzi umekamilika. Skimu zitakazokarabatiwa ni Mvumi, Kilosa (hekta 260); Musa Mwinjanga, Hai (hekta 641); Katuka, Sumbawanga (hekta 100); Muhwazi, Kibondo (hekta 100); Bugorora, Ukerewe (hekta 200); Kalemela, Magu (hekta 20); Mbarika, Misungwi (hekta 45) na Kalenga, Iringa (240). Aidha, Wizara itahimiza uanzishaji wa vyama vya umwagiliaji maji mashambani na vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa katika skimu za Buswahili (Musoma), Balili (Bunda), Ochuna (Tarime), Lumuma (Kilosa), Ruvu (Kibaha) na skimu ya Bagamoyo. Miradi hii itakarabatiwa kwa fedha za serikali zilizotengwa kwenye bajeti ya mwaka wa 2002/2003.

### Mradi wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani katika Mabonde ya Mito Pangani na Rufiji

**92.** Mradi huu unatekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia na mchango wa serikali ya Tanzania na nguvu za wananchi. Katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, Wizara ya Kilimo na Chakula itakamilisha ujenzi wa miradi minne ambayo haikukamilika katika mwaka wa 2001/2002 na kuanzisha vishamba vya mfano katika miradi hiyo. Miradi hiyo ni Kivulini, Mwanga (hekta 410); Long'oi, Hai (hekta 300); Mapogoro, Iringa (hekta 350) na Nyamahana, Iringa (hekta 109). Aidha, mradi utasaidia baadhi ya wakulima kuzalisha mbegu za mpunga katika skimu 4 za Igomelo (Mbarali), Luganga (Iringa), Lekitatu (Arumeru) na Mombo (Korogwe).

### Miradi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani Chini ya Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo (*Agriculture Sector Programme Support – ASPS*)

**93.** Katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, Wizara ya Kilimo na Chakula, itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani katika miradi ya Lumuma, Kilosa (hekta 960) na Nyanzwa, Iringa vijijini (hekta 760). Aidha, Wizara itawahamasisha wakulima kuchangia nguvukazi katika ujenzi wa skimu hizo na kutoa mafunzo ya umwagiliaji maji mashambani kuhusu matumizi bora ya maji. Miradi hii inafadhiliwa na serikali ya Denmark.

### Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani (*Participatory Irrigation Development Programme – PIDP*)

**94.** Katika mwaka wa 2002/2003, jumla ya skimu 18 zitaendelezwa katika wilaya sita za Babati, Dodoma Vijijini, Kwimba, Manyoni, Nzega na Shinyanga (*Kiambatanisho Na. 8*). Kila wilaya itakuwa na skimu tatu. Kazi zitakazofanyika ni kujenga miundombinu ya umwangiliaji maji mashambani, kuchimba malambo ya kuvuna maji na kuchimba visima vifupi. Aidha, mradi utasaidia wakulima kuunda na kuimarisha vikundi vya wamwagiliaji maji mashambani na kutoa mafunzo kwa wakulima na Maafisa Ugani katika skimu hizo. Mradi huu unafadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Serikali ya Ireland na Mpango wa Chakula Duniani (WFP).

### Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani wa Lower Moshi – Awamu ya Pili

**95.** Awamu ya kwanza ya mradi huu iliendeleza jumla ya hekta 2,300. Mavuno ya mpunga katika mradi huu yamefikia wastani wa tani 6.5 kwa hekta kutoka tani 1.5 kwa hekta zilizokuwa zikizalishwa kabla ya mradi. Lengo la awamu ya pili ni kuongeza hekta 2,400. Katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, Wizara ya Kilimo na Chakula itashirikina na Wizara za Maji na Maendeleo ya Mifugo na Madini na Nishati kutatua mgogoro uliopo juu ya matumizi ya maji ya Mto Kikavu ili awamu ya pili ya mradi iweze kutekelezwa.

## Mpango Kabambe wa Taifa wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani (*National Irrigation Master Plan study – NIMP*)

**96.** Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani kwa msaada wa serikali ya Japan, yalianza mwezi wa Oktoba, 2001 na yanatarajiwa kukamilika mwezi wa Machi, 2004. Maandalizi ya Mpango huo yanafanywa na timu ya wataalam wa Wizara ya Kilimo na Chakula na wataalam kutoka Japan. Katika mwaka wa 2002/2003, timu hiyo itafanya kazi za kubainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani katika nchi nzima. Timu hiyo ya wataalam itakusanya na kuchambua takwimu na taarifa zilizopo juu ya kilimo cha umwagiliaji maji mashambani ili kubaini matatizo yanayokwamisha ukuaji wa kilimo hicho na kupendekeza mbinu za kuyatatua. Aidha, Halmashauri za wilaya zote nchini zitakamilisha kuandaa orodha ya miradi ya kilimo cha umwagiliaji maji mashambani itakayopewa kipaumbele katika utekelezaji.

### HUDUMA ZA UGANI

**97.** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula, itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuhakikisha kwamba huduma za Ugani zinaimarika. Ili kufanikisha azma hiyo, Wizara itafanya yafuatayo:

- Kuendeleza matumizi ya Mbinu *Shirikishi Jamii* na *Shamba Darasa,* kama mbinu za kuwawezesha wakulima kuelewa vizuri zaidi teknolojia za kilimo na jinsi ya kuzisambaza kwa wakulima wengine. Katika mwaka wa 2002/2003, mbinu hizi zitaendelezwa na kutumika katika mikoa yote . Hivyo, mafunzo yatatolewa kwa viongozi wote wa mikoa na wilaya na wataalam wote wa kilimo, ili kuwawezesha kuwaandaa na kuwafundisha wakulima mbinu hizo.
- Kuwaelimisha wakulima mbinu bora za kilimo kupitia vipindi vya redio na vijarida. Jumla ya vipindi 125 kuhusu kilimo bora, lishe bora, hifadhi ya chakula na utunzaji wa miti vitatangazwa redioni.
- Kutoa mafunzo kwa wakulima, juu ya mbinu bora za kilimo zenye mwelekeo wa kibiashara kwa kutumia vyuo vya kilimo, vituo vya Utafiti na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii.
- Kushirikiana na Halmashauri za wilaya za Kisarawe na Mkuranga kukamilisha ujenzi wa ofisi za kilimo na Halmashauri za wilaya za Nachingwea, Lindi, Tandahimba na Mtwara Mjini kujenga nyumba nne za maafisa ugani.
- Kununua magari 50 na baiskeli 1,200. Vifaa hivi vya usafiri vitasambazwa wilayani ili kuwawezesha wataalam kuwafikia wakulima na kutoa huduma za kitaalam.

## Mradi wa Kuongeza Rutuba kwenye Udongo na Tija katika Kilimo (*Soil Fertility Recapitalization and Agricultural Intensification Project – SOFRAIP*)

**98.** Mheshimiwa Spika, mradi wa SOFRAIP utasaidia wakulima kutekeleza miradi wanayobuni wenyewe na kujenga uwezo wa watekelezaji wa mradi katika ngazi zote. Halmashauri za wilaya zitawasaidia wakulima kuandaa mipango kazi na kufuatilia utekelezaji. SOFRAIP itachangia fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mipango hiyo.

**99.** Wilaya nane za Arumeru, Hai, Hanang, Iringa, Masasi, Morogoro, Nachingwea na Singida zitaanza kutekeleza mradi kuanzia mwaka huu wa fedha. Wilaya za Hai na Morogoro zimechaguliwa kutekeleza mradi kwa majaribio. Uzoefu utakaopatikana utatumiwa katika utekelezaji unaokusudiwa na mradi. Majaribio hayo ni muhimu katika kukamilisha maandalizi ya mradi kabla ya kufanya tathmini (*appraisal*) ambayo inatarajiwa kufanyika kabla ya mwisho wa mwaka wa 2002.

### Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea na Mazao

**100.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara ya Kilimo na Chakula, itaendelea kutekeleza yafuatayo:

- Kuendeleza Programu ya *Udhibiti Husishi* wa visumbufu vya mimea kama njia yenye gharama nafuu, endelevu na salama. Programu hiyo itatekelezwa katika mikoa ya Shinyanga, Arusha, Mbeya, Iringa, Ruvuma, Rukwa, Dodoma, Singida na Morogoro.
- Kushirikiana na mashirika ya kimataifa yanayodhibiti nzige na Kwelea kwelea katika kukagua mazalio ya visumbufu hivyo na kuvidhibiti mapema ili kuokoa mazao ya wakulima. Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kulipa ada za uanachama katika mashirika hayo.
- Kuimarisha miundombinu ya utabiri wa milipuko ya visumbufu.
- Kuimarisha uwezo wa wataalam kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea *(Plant Protection Act, 1997)* kwa kutoa mafunzo na vifaa. Aidha, Wizara itarekebisha sheria ya TPRI ya mwaka wa 1979 ili iwiane na sheria nyingine, hususan Sheria ya Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea.

### Mafunzo ya Kilimo kwa Wataalum na Wakulima

**101.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003 kazi zitakazofanyika ni pamoja na:

- Kurekebisha mitaala mitano ili kuingiza vipengele muhimu vya kilimo cha biashara, mazingira na elimu ya UKIMWI. Aidha, Wizara itaendesha mafunzo rejea ya mazao ya kahawa, pamba na korosho kwa maafisa ugani vijijini wapatao 300. Mafunzo yatatolewa pia kwa wataalam bingwa wapatao 30 juu ya kanuni bora za uzalishaji wa mazao hayo, kwa lengo la kuwafundisha mabwana shamba.
- Kudhamini mafunzo ya wataalam wa kilimo 200 wenye astashahada kuchukua mafunzo ya stashahada katika fani za kilimo (150). Umwagiliaji Maji Mashambani (25) na matumizi ya zana bora za kilimo (25). Aidha, vyuo vya kilimo kwa kushirikiana na mashirika mbalimbali, na kwa ufadhili wa Wizara, vitatoa mafunzo kwa wakulima 4,500 juu ya kanuni bora za kilimo na kilimo cha kutumia wanyamakazi.
- Kutayarisha vitabu vya aina tano kuhusu kanuni bora za kilimo kwa ajili ya matumizi vyuoni, wakulima na maafisa ugani.
- Kuimarisha mafunzo ya kilimo cha umwagiliaji maji mashambani kwa wakulima katika vyuo vya kilimo na vyuo vya wakulima.
- Kuimarisha mafunzo ya wanyama kazi na matumizi ya zana za kilimo vyuoni.
- Aidha, Vyuo vya kilimo vitaendelea kutekeleza shughuli zake kibiashara kwa kuuza programu za mafunzo ya wakulima kwa taasisi, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na wafadhili ambao wako tayari kuendeleza sekta ya kilimo kama vile *Heifer Project International, CARITAS, CARE International na World Vision Tanzania.*

### Matumizi ya Pembejeo na Zana za Kilimo

**102.** Mheshimiwa Spika, kilimo chetu bado kinategemea zaidi jembe la mkono ambalo linarudisha nyuma uwezo wa wakulima kuongeza maeneo wanayolima. Ili kuwawezesha wakulima wetu kupanua maeneo wanayolima na kukamilisha kazi zao za mashambani kwa haraka na kwa ufanisi ni muhimu kutumia zana bora zinazokokotwa na wanyama kazi au matrekta. Wakati kaya moja yenye watu watano ina uwezo wa kulima hekta mbili kwa msimu kwa kutumia jembe la mkono, kaya moja yenye jozi moja ya maksai inaweza kulima hekta tano hadi nane kwa msimu. Hivyo, matumizi ya wanyama kazi yanaweza kupanua eneo linalolimwa na wakulima kwa kiasi kikubwa. Katika mwaka wa 2002/2003, Wizara ya Kilimo na

Chakula imeweka msukumo zaidi katika kupanua kilimo cha maksai na imetenga shilingi milioni 300 kuendeleza kilimo hicho kwa kuwa gharama zake ni nafuu zaidi kulinganisha na matrekta na hivyo wakulima wengi hususan wakulima wadogo wanaweza kumudu. Mikoa yenye mifugo mingi ya Shinyanga, Mwanza, Mara, Tabora, Singida, Dodoma, Arusha, Mbeya, Iringa na Rukwa itapewa kipaumbele.

**103.** Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Mashirika yasiyo ya kiserikali na Sekta binafsi itatekeleza kazi zifuatazo: -

- Kutoa mafunzo ya matumizi ya zana bora zinazokokotwa na wanyama kazi kwa wakulima 300 wa mfano na mabwana shamba 120 kutoka mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Tabora, Singida, Dodoma, Arusha, Mbeya, Iringa, Rukwa, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro na Mtwara. Mafunzo hayo yatatolewa katika vyuo vya kilimo, vituo vya maksai na vyuo vya wakulima. Wakulima hao wa mfano na mabwana shamba wataunda timu za wataalam watakaotoa mafunzo kwa wakulima vijijini. Wakulima 6,000 watapata mafunzo chini ya utaratibu huo.
- Kukarabati vituo 20 vya maksai na kuvipatia zana bora, kama vile majembe ya palizi, *"magoye ripper"*, mashine za kupanda mbegu na mikokoteni. Vituo hivyo vitatoa mafunzo kwa wakulima, wahunzi na mafundi vijijini juu ya matumizi, matunzo na matengezo ya zana hizo.
- Kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha na kuendesha vituo vya kukodisha matrekta ili waweze kutoa huduma hiyo kwa wakulima wengi zaidi. Aidha, mafundi sanifu 80 kutoka mikoa ya Mwanza, Kagera, Kigoma, Tabora, Dodoma, Mbeya, Rukwa, Lindi, Mtwara, Iringa, Singida na Tanga watapata mafunzo kuhusu matumizi, matunzo na matengenezo ya matrekta madogo ya mkono, ili kuwawezesha kutoa huduma hiyo kwa wakulima.

### Mbegu

**104.** Mheshimiwa Spika, makisio ya mahitaji ya mbegu zilizothibitishwa katika msimu wa 2002/2003 ni tani 30,000. Upatikanaji wa mbegu unategemewa kuwa tani 12,500. Kati ya hizo, kampuni binafsi za mbegu zitazalisha tani 6,000 na kuingiza nchini tani 4,000. Mashamba ya Serikali ya Mbegu ya Dabaga, Arusha, Msimba, Kilangali na Mwele yanatarajiwa kuzalisha jumla ya tani 1,500 za mbegu. Aidha, chini ya mfumo wa uzalishaji mbegu kwa kutumia wakulima wadogo, tani 1,000 za mbegu zinatarajiwa kuzalishwa katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Iringa, Lindi, Mtwara na Pwani, ambapo jumla ya vijiji 222 vitahusishwa. Udhibiti wa ubora wa mbegu vijijini, utaimarishwa kwa kutoa mafunzo kwa maafisa ugani 20 kutoka mikoa ya Morogoro, Dodoma, Iringa, Arusha, Mbeya na Shinyanga.

### Mbolea na Madawa

**105.** Makisio ya mahitaji ya mbolea kwa mwaka wa 2002/2003 ni tani 185,500, madawa ya unga ni tani 21,000 na madawa ya maji ni lita milioni nne. Ili kuingiza pembejeo za kilimo zenye ubora unaokubalika na kuzisambaza kwa wakulima kwa wakati unaofaa, Wizara ya Kilimo na Chakula, itaendelea kuwahamasisha wafanyabiashara kuagiza pembejeo zinazotakiwa mapema na kuzisambaza. Aidha, Wizara itaendelea kuwahamasisha wafanyabiashara hao, kufunga mbolea katika ujazo mdogo ili wakulima wamudu kuzinunua.

### Mfuko wa Pembejeo

**106.** Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2002/2003 Mfuko wa Pembejeo utaanza tena kutoa mikopo kwa ajili ya kuagiza na kusambaza pembejeo na zana za kilimo baada ya kukamilika kwa maandalizi ya utaratibu wa kutoa mikopo hiyo kupitia kwenye vyombo vya fedha. Mikopo hiyo itatolewa kwa masharti ya ukopeshaji ya Benki na wakopaji watapaswa kurejesha mikopo watakayopewa kwa utaratibu watakaokubaliana na Benki. Mikopo ya Mfuko wa Pembejeo itakuwa na riba ndogo kuliko ile inayotozwa

na mabenki kwa mikopo yao ya kawaida ili kuwawezesha wakulima kupata pembejeo kwa bei nafuu. Sambamba na utoaji wa mikopo, Mfuko wa Pembejeo utatoa mafunzo kwa mawakala wa mfuko kuhusu utunzaji na matumizi bora ya pembejeo na zana.

**107.** Mfuko umeandaa utaratibu na aina ya mtandao wa usambazaji wa pembejeo ambao utawezesha wakulima kupata pembejeo na zana kwa wakati na kwa bei nafuu. Chini ya utaratibu huo, Mfuko umekubaliana na Benki ya Ushirika Kilimanjaro na *Exim Bank (T) Ltd*., kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wauza pembejeo na vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa vyenye uongozi mzuri, hususan vinavyohudumiwa na benki ya CRDB. Mfuko utashirikiana na mabenki hayo na Halmashauri za Wilaya, kufuatilia na kuhakikisha kuwa mawakala wa Mfuko wanafikisha pembejeo vijijini kwa wakulima kwa wakati na kuziuza kwa bei nafuu. Wizara itaainisha taasisi nyingine za fedha zitakazojumuishwa katika kutoa mikopo chini ya utaratibu huu.

### HIFADHI YA UDONGO NA MAJI

**108.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara ya Kilimo na Chakula, itashirikiana na Halmashauri za Wilaya za Kigoma Vijijini, Magu na Korogwe kuendeleza na kueneza mbinu na teknolojia endelevu za hifadhi ya udongo na maji, kwa kutoa mafunzo kwa maafisa ugani 40 na wakulima 120, ili waendeleze mafunzo hayo kwa wakulima wengi vijijini. Maeneo mapya yaliyoathiriwa na mmomonyoko wa udongo yatabainishwa na mipango ya ukarabati kuandaliwa katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Rukwa, Singida, Dodoma na Shinyanga.

**109.** Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Mradi wa Hifadhi Mazingira ya Ziwa Viktoria itaendelea kushirikiana na Halmashauri za mikoa ya Mwanza, Mara na Shinyanga kutekeleza mikakati ya kuzuia mmomonyoko wa udongo. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha wakulima kutekeleza mbinu bora za kuhifadhi ardhi na kurutubisha udongo, katika tarafa za Isimani (Iringa Vijijini) na Mikese (Morogoro Vijijini).

### HIFADHI NA USALAMA WA CHAKULA

## Usalama wa Chakula

**110.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara ya Kilimo na Chakula itaendelea kuratibu taarifa za hali ya hewa na mazingira ya uzalishaji wa mazao, kufanya tathmini ya hali ya chakula katika ngazi za taifa, mikoa na wilaya na kuandaa na kusambaza taarifa za upatikanaji wa chakula nchini. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati ya kupunguza upotevu wa mavuno. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na:

- Kuainisha teknolojia za hifadhi za mazao muhimu ya chakula yaani nafaka, mikunde, mboga na matunda, mazao ya mafuta, na mazao ya aina ya mizizi na kuziboresha.
- Kuainisha wadau na kuwashirikisha katika kuboresha mfumo wa hifadhi ya chakula.
- Kutengeneza miongozo juu ya njia bora za kuzuia upotevu wa mazao na kuhakikisha inasambazwa kwa wadau.
- Kuandaa vitabu na vipeperushi vya jinsi ya kupunguza upotevu wa mavuno kwa kila zao.
- Kuimarisha uwezo wa Wizara wa kufundisha wataalam wa ugani na wakulima kuhusu teknolojia rahisi za kukabiliana na upotevu wa mazao baada ya mavuno.
- Kuratibu taarifa za hali ya hewa na mazingira ya uzalishaji wa mazao, kufanya tathmini za hali ya chakula katika ngazi za Taifa, mikoa na wilaya na kuchambua, kuandaa na kusambaza taarifa za upatikanaji wa chakula nchini. Lengo ni kuboresha uwezo wa kutoa tahadhari za upungufu wa chakula kwa wakati mwafaka, ili kuepusha baa la njaa.

- Kuandaa sera ya usalama na uhakika wa chakula.

### Hifadhi ya Chakula

**111.** Mheshimwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, Hifadhi ya Chakula ya Taifa inakusudia kununua akiba ya chakula ya jumla ya tani 20,900 za mahindi kutoka hapa nchini. Kati ya hizo, tani 16,400 zitanunuliwa kutokana na shilingi bilioni 1.9, fedha zilizotengwa na Hazina kwenye bajeti hii ya mwaka wa 2002/2003, na tani 4,500 zitanunuliwa kutokana na shilingi milioni 500 za mauzo ya mahindi ya Hifadhi ya Chakula ya Taifa ya msimu uliotangulia wa 2001/2002. Hifadhi ya Chakula inakusudia kununua mahindi kutoka kwenye maeneo yenye ziada kulingana na uwezo.

#### Ubinafsishaji wa Mashirika ya Kilimo

**112.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, mashirika na mashamba yafuatayo yatabinafsishwa: - mali zilizobaki za Shirika la Usagishaji la Taifa (NMC), yakiwemo maghala 22, vinu vitatu vilivyoko Isaka, Tabora na Shinyanga; mashamba ya NAFCO ya ngano na mpunga, jineri ya Bodi ya Pamba iliyoko Manawa; Kampuni ya Kahawa ya TANICA, Kiwanda cha Chai cha Lupembe; shamba la chai la Mlangali; viwanda 12 vya korosho na mashamba ya mkonge.

#### Maendeleo ya Watumishi

**113.** Mheshimiwa spika, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara ya Kilimo na Chakula, itaendelea kuwapandisha vyeo watumishi 1,041 waliobakia katika awamu ya kwanza na kuendelea kuwapandisha vyeo viwili viwili watumishi ambao watakuwa hawajafikia kikomo cha miundo yao ya utumishi.

Sambamba na kazi hiyo Wizara itaendelea na utekelezaji wa mikakati iliyojiwekea ya kupiga vita **rushwa na ugonjwa wa ukimwi**.

## V. HITIMISHO

**114.** Mheshimiwa Spika, kilimo ndiyo kazi kuu ya uchumi kwa asilimia 80 ya Watanzania. Upunguzaji wa umaskini utategemea kwa kiasi kikubwa maendeleo ya kilimo. Nchi yetu ina uwezo mkubwa sana wa kupanua kilimo chake kutokana na raslimali zilizopo.

**115.** Sekta ya kilimo inategemewa kukua kwa kasi kubwa zaidi kwa miaka ijayo kutokana na uwekezaji unaotarajiwa kufanywa katika maeneo yanayomnufaisha mkulima moja kwa moja na katika mambo yenye uwezekano wa kutoa mafanikio katika kipindi kifupi, kuruhusiwa kwa uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi, ushindani wa soko huria na uhamasishaji wa wakulima katika ngazi zote. Mazao yanategemewa kuchangia zaidi ya asilimia 75 ya ukuaji wa sekta ikilinganishwa na mchango wa asilimia 70 wa ukuaji wa mwaka wa 2001. Hata hivyo, mafanikio ya kuendeleza kilimo yatategemea ushirikiano wa wadau wote wa sekta ya kilimo hususan Halmashauri za Wilaya.

## VI. SHUKRANI

**116.** Aidha, napenda kuzishukuru nchi na Mashirika ya Kimataifa yafuatayo, ambayo yanaendelea kuisaidia Wizara ya Kilimo na Chakula, katika juhudi za kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo. Nchi hizo ni Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Israeli, Italia, Japan, Korea Kusini, Marekani, Misri, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi na Sweden. Vile vile napenda

kuyashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo:- Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi Afrika, JICA, DFID, NRI, USAID, GTZ, UNDP, FAO, EU, UNICEF, WFP, IFAD, CIMMYT, ICRAF, ICRISAT, ASARECA, IITA na Sasakawa Global 2000. Bado tunahitaji ushirikiano wao ili kuendeleza kilimo nchini.

**117.** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa wakulima wa Tanzania, kwa kuwa wachangiaji wakuu wa pato la Taifa, kutokana na kazi nzuri wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Pamoja na mazingira magumu ya uzalishaji, kama vile ukosefu wa pembejeo muhimu, teknolojia duni na kilimo cha kutegemea mvua, wameliwezesha Taifa letu kujitegemea kwa chakula kwa zaidi ya asilimia 97. Aidha, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wadau wote wa sekta ya kilimo kwa michango yao ambayo imeiwezesha Wizara ya Kilimo na Chakula kutekeleza mambo mengi kwa ufanisi mkubwa.

## VII. MAOMBI YA FEDHA 2002/2003

**118.** Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe shilingi 14,658,874,900 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 18,603,608,100 kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, shilingi 1,823,818,200 ni fedha za hapa na shilingi 16,779,789,900 fedha za nje.

**119. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.**

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| ASARECA | = | Association for Strengthening Agricultural Research in East and Central Africa |
| ASPS | = | Agricultural Sector Programme Support |
| CFC | = | Common Fund for Commodities |
| CIMMYT | = | *Shirika la Kimataifa la Utafiti wa Ngano na Mahindi* |
| DANIDA | = | Danish International Development Agency |
| DFID | = | Department for International Development |
| EU | = | European Union |
| FAO | = | Food and Agriculture Organization |
| GAPEX | = | General Agricultural Product for Export |
| GTZ | = | *German Agency for International Cooperation* |
| ICRAF | = | International Centre for Research in Agroforestry |
| ICRISAT | = | International Centre for Research for Arid and Semi Arid Tropics |
| IFAD | = | International Fund for Agricultural Development |
| IITA | = | International Institute of Tropical Agriculture |
| IPM | = | Integrated Pest Management |
| JICA | = | Japan International Cooperation Agency |
| KATC | = | Kilimanjaro Agricultural Training Centre |
| NAEP II | = | National Agricultural Extension Project II |
| NAFCO | = | National Agriculture and Food Company |
| NMC | = | National Milling Corporation |
| NRI | = | National Resources Institute |
| SACCOs | = | Savings and Credit Co-operatives Societies |
| SADC | = | Southern Africa Development Co-operation |
| SOFRAIP | = | Soil Fertility Recapitalization and Agricultural Intensification Project |
| TACRI | = | Tanzania Coffee Research Institute |
| TANICA | = | Tanganyika Instant Coffee Company Ltd |
| TANSEED | = | Tanzania Seed Company Ltd |
| TARP II | = | Tanzania Agricultural Research Project II |
| TASO | = | Tanzania Agricultural Society |
| TORITA | = | Tobacco Research Institute of Tanzania |
| TPRI | = | Tropical Pesticides Research Institute |
| TRIT | = | Tea Reseach Institute of Tanzania |
| WFP | = | World Food Programme |

**Kiambatanisho Na 1: Hali ya Tija kwa baadhi ya Mazao ya Kilimo**

| | ZAO | Tija ilivyo sasa (Kg/ha) | Tija inayowezekana (Kg/ha) |
|---|---|---|---|
| **1** | Mahindi | 600-2,200 (Katika mikoa isiyozalisha mahindi kwa wingi) | |
| | | 1,000-3,000 (Katika mikoa inayozalisha mahindi kwa wingi kama Ruvuma, Rukwa, Mbeya na Iringa). | 5,000 |
| **2** | Mpunga | 2,900 (Katika maeneo yanayotegemea kilimo cha mvua) | 4,000-5,000 |
| | | 4,500 (Kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji maji mashambani) | 6,000 |
| **3** | Mtama na Uwele | 640 | 1,200 |
| **4** | Muhogo | 8,000-12,000 | 20,000-25,000 |
| **5** | Mikunde | 700 | 1,500-3,000 |
| **6** | Ngano | 800-1,000 | 3,000 |
| **7** | Maharage | 200-700 | 1,500-3,000 |
| **8** | Viazi | 8,000-10,000 | 20,000-30,000 |
| **9** | Ndizi | 9,000 | 25,000-35,000 |
| **MAZAO YA BIASHARA** | | | |
| **1** | Kahawa | 100-170 | 550-600 |
| **2** | **Pamba** | | |
| | Kanda ya Mashariki | 500 | 1,400 |
| | Kanda ya Magharibi | 500 | 1,400 |
| **3** | **Tumbaku** | | |
| | Tumbaku ya mvuke | 950-1000 | 1,800 |
| | Tumbaku ya moshi | 950 | 1,800 |
| **4** | **Chai** | | |
| | Mashamba makubwa | 3,500 | 5,500 |
| | Wakulima wadogo | 470 | 3,000 |
| **5** | Miwa | | |
| | Mashamba makubwa | 75,000 | 120,000 |
| | Wakulima wadogo | 70,000 | 110,000 |
| **6** | **Mbegu za mafuta** | | |
| | Alizeti | 300 | 1,200 |
| | Ufuta | 300 | 1,200 |
| | Karanga | 600 | 1,500 |
| | Michikichi | 500-600 | 2,500 |
| | Maharage ya Soya | 500 | 1,500-3,000 |
| **7** | Korosho | 400-500 | 1,200-1,300 |
| **8** | Mkonge | 1000 | 1,500 |
| **9** | Pareto | 300 | 600 |

*Chanzo: Wizara ya Kilimo na Chakula*

**Kiambatanisho 2A: Uchambuzi wa Hali ya Chakula kwa mwaka 2002/03 (Tani)** (Kutokana na Tathmini ya ya awali ya mavuno (*Preliminary forecast*) ya 2001/2002))

| Mkoa | Matarajio ya Mazao ya Nafaka | | | | Matarajio ya Mazao Yasiyo Nafaka | | | | Jumla ya Matarajio ya Mavuno Yote | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mavuno | Mahitaji | Upungufu-/ Ziada | Kiwango cha Kujitoshelez a (Nafaka - %) | Mavuno | Mahitaji | Upungufu -/ Ziada | Kiwango cha Kujitoshelez a (Yasiyo Nafaka - %) | Mavuno | Mahitaji | Upungufu / Ziada | Kiwango cha Kujitoshelez a (Chakula %) |
| Arusha | 258,200 | 372,708 | -114,507 | **69** | 173,810 | 225,983 | -52,174 | **77** | 432,010 | 598,691 | -166,681 | **72*** |
| Coast | 74,902 | 196,088 | -121,186 | **38** | 254,135 | 119,047 | 135,088 | **213** | 329,037 | 315,135 | 13,903 | **104** |
| Dar es Salaam | 7,724 | 388,322 | -380,598 | **2** | 32,662 | 253,920 | -221,258 | **13** | 40,386 | 642,242 | -601,856 | **6*** |
| Dodoma | 262,952 | 268,635 | -5,683 | **98** | 171,312 | 165,531 | 5,781 | **103** | 434,264 | 434,166 | 98 | **100** |
| Iringa | 402,226 | 273,218 | 129,008 | **147** | 161,736 | 168,904 | -7,167 | **96** | 563,963 | 442,122 | 121,841 | **128** |
| Kagera | 126,817 | 277,064 | -150,247 | **46** | 482,329 | 190,300 | 292,029 | **253** | 609,145 | 467,364 | 141,781 | **130** |
| Kigoma | 162,123 | 173,587 | -11,464 | **93** | 154,371 | 121,898 | 32,473 | **127** | 316,494 | 295,485 | 21,009 | **107** |
| Kilimanjaro | 195,677 | 217,071 | -21,394 | **90** | 152,508 | 141,869 | 10,639 | **107** | 348,185 | 358,940 | -10,755 | **97*** |
| Lindi | 100,892 | 176,740 | -75,848 | **57** | 171,644 | 81,525 | 90,119 | **211** | 272,537 | 258,265 | 14,271 | **106** |
| Mara | 190,571 | 222,625 | -32,054 | **86** | 205,739 | 139,672 | 66,067 | **147** | 396,310 | 362,297 | 34,013 | **109** |
| Mbeya | 405,707 | 333,602 | 72,105 | **122** | 229,774 | 218,631 | 11,142 | **105** | 635,481 | 552,234 | 83,247 | **115** |
| Morogoro | 289,064 | 264,102 | 24,963 | **109** | 181,627 | 173,084 | 8,544 | **105** | 470,691 | 437,185 | 33,506 | **108** |
| Mtwara | 98,829 | 156,645 | -57,816 | **63** | 304,784 | 102,659 | 202,125 | **297** | 403,613 | 259,304 | 144,308 | **156** |
| Mwanza | 325,577 | 394,740 | -69,163 | **82** | 422,979 | 258,699 | 164,279 | **164** | 748,555 | 653,439 | 95,116 | **115** |
| Rukwa | 318,548 | 192,272 | 126,276 | **166** | 95,388 | 126,009 | -30,621 | **76** | 413,936 | 318,281 | 95,655 | **130** |
| Ruvuma | 186,860 | 179,615 | 7,245 | **104** | 180,236 | 117,714 | 62,522 | **153** | 367,096 | 297,328 | 69,767 | **123** |
| Shinyanga | 443,836 | 389,140 | 54,695 | **114** | 237,805 | 255,029 | -17,224 | **93** | 681,641 | 644,170 | 37,471 | **106** |
| Singida | 166,912 | 163,940 | 2,972 | **102** | 109,554 | 107,441 | 2,114 | **102** | 276,467 | 271,381 | 5,086 | **102** |
| Tabora | 212,430 | 211,439 | 990 | **100** | 124,576 | 138,570 | -13,994 | **90** | 337,005 | 350,009 | -13,004 | **96*** |
| Tanga | 210,771 | 255,867 | -45,096 | **82** | 259,826 | 167,687 | 92,140 | **155** | 470,597 | 423,553 | 47,044 | **111** |
| **Jumla** | **4,440,617** | **5,107,421** | **-666,804** | **87** | **4,106,795** | **3,274,172** | **832,623** | **125** | **8,547,412** | **8,381,593** | **165,819** | **102** |

**Angalia: *** Ishara ya kutarajiwa kwa upungufu wa chakula.

***Chanzo: Wizara ya Kilimo***

**Kiambatanisho Na. 2B: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula tangu mwaka 1986/87 –2000/2001 (Tani ‘000**

| Mwaka | Mahindi | Mpunga | Ngano | Mtama/ Uwele | Jumla Nafaka | Mikunde | Mhogo | Viazi vitamu | Ndizi | Jumla Mazao yasiyo nafaka | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 19986/87 | 2,359 | 419 | 72 | 954 | 3,804 | 251 | 1,709 | 336 | 792 | 3,088 | **6,892** |
| 1987/88 | 2,339 | 400 | 76 | 682 | 3,497 | 379 | 1,736 | 319 | 812 | 3,246 | **6,743** |
| 1988/89 | 3,125 | 468 | 97 | 804 | 4,494 | 385 | 1,948 | 337 | 743 | 3,413 | **7,907** |
| 1989/90 | 2,445 | 481 | 106 | 568 | 3,600 | 388 | 1,724 | 1,023 | 823 | 3,958 | **7,558** |
| 1990/91 | 2,332 | 406 | 84 | 750 | 3,572 | 425 | 1,566 | 291 | 750 | 3,032 | **6,604** |
| 1991/92 | 2,226 | 256 | 64 | 850 | 3,396 | 312 | 1,778 | 257 | 794 | 3,141 | **6,737** |
| 1992/93 | 2,282 | 417 | 59 | 929 | 3,687 | 406 | 1,708 | 260 | 800 | 3,174 | **6,861** |
| 1993/94 | 2,159 | 399 | 59 | 696 | 3,313 | 187 | 1,802 | 267 | 734 | 3,090 | **6,403** |
| 1994/95 | 2,567 | 470 | 75 | 1,250 | 4,362 | 378 | 1,492 | 451 | 651 | 2,972 | **7.334** |
| 1995/96 | 2,663 | 477 | 84 | 1,239 | 4,463 | 475 | 1,498 | 420 | 641 | 3,034 | **7,497** |
| 1996/97 | 1,831 | 357 | 78 | 845 | 3,112 | 374 | 1,426 | 372 | 603 | 2,776 | **5,888** |
| 1997/98 | 2,685 | 676 | 111 | 799 | 4,271 | 762 | 1,758 | 644 | 836 | 3,700 | **7,972** |
| 1998/99 | 2,452 | 506 | 82 | 755 | 3,796 | 526 | 1,795 | 570 | 752 | 3,645 | **7,440** |
| 1999/2000 | 2,009 | 508 | 33 | 817 | 3,368 | 674 | 1,781 | 798 | 703 | 3,935 | **7,322** |
| 2000/2001 | 2,579 | 564 | 89 | 906 | 4,141 | 733 | 1,445 | 596 | 779 | 3,553 | **7,695** |
| Wastani miaka 14 | 2,403 | 454 | 78 | 857 | 3,792 | 424 | 1,678 | 463 | 754 | 3,318 | **7,110** |

*Chanzo: Wizara ya Kilimo*

**Kiambatanisho Na. 2C: Uzalishaji wa Chakula (2000/2001-2001/2002) na Mahitaji ya Chakula Nchini 2002/2003 (Tani)**

| | 2001/2002 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Nafaka | | | MazaoYasiyo Nafaka | | | Jumla | | | |
| Mkoa | Uzalishaji | Mahitaji | Ziada/ Upungufu | Uzalishaji | Mahitaji | | Uzalishaji | Mahitaji | Ziada/ Upungufu | Asilimia ya |
| Arusha | 260,940 | 359,822 | **-98,882** | 158,603 | 218,465 | **-59,862** | 419,543 | 578,287 | **-158,745** | 73 |
| DSM* | | | **0** | | | **0** | 0 | 0 | **0** | |
| Pwani * | 104,431 | 553,668 | **-449,237** | 269,114 | 356,226 | **-87,112** | 373,545 | 909,894 | **-536,348** | 41 |
| Dodoma | 199,688 | 265,459 | **-65,772** | 99,922 | 163,159 | **-63,237** | 299,610 | 428,619 | **-129,009** | 70 |
| Iringa | 392,468 | 286,268 | **106,200** | 129,827 | 164,463 | **-34,636** | 522,294 | 450,731 | **71,564** | 116 |
| Kagera | 122,545 | 287,791 | **-165,245** | 459,430 | 185,297 | **274,133** | 581,975 | 473,087 | **108,888** | 123 |
| Kigoma | 156,220 | 180,933 | **-24,713** | 150,730 | 118,577 | **32,153** | 306,950 | 299,510 | **7,440** | 102 |
| K’njaro | 191,107 | 213,284 | **-22,177** | 147,859 | 138,951 | **8,908** | 338,966 | 352,234 | **-13,268** | 96 |
| Lindi | 96,926 | 124,028 | **-27,101** | 147,219 | 79,927 | **67,292** | 244,145 | 203,954 | **40,190** | 120 |
| Mara | 179,952 | 216,382 | **-36,430** | 180,808 | 135,737 | **45,072** | 360,760 | 352,119 | **8,641** | 102 |
| Mbeya | 380,924 | 323,571 | **57,353** | 196,282 | 212,057 | **-15,775** | 577,206 | 535,629 | **41,577** | 108 |
| Morogoro | 271,237 | 257,409 | **13,828** | 162,762 | 168,697 | **-5,935** | 433,998 | 426,106 | **7,893** | 102 |
| Mtwara | 91,991 | 154,482 | **-62,491** | 253,947 | 101,242 | **152,705** | 345,938 | 255,724 | **90,214** | 135 |
| Mwanza | 305,307 | 384,737 | **-79,430** | 358,568 | 252,143 | **106,425** | 663,876 | 636,880 | **26,996** | 104 |
| Rukwa | 301,590 | 183,993 | **117,597** | 89,948 | 120,582 | **-30,634** | 391,539 | 304,575 | **86,964** | 129 |
| Ruvuma | 179,950 | 174,045 | **5,905** | 156,947 | 114,063 | **42,884** | 336,897 | 288,109 | **48,788** | 117 |
| S’yanga | 414,208 | 378,173 | **36,034** | 198,648 | 247,842 | **-49,194** | 612,856 | 626,016 | **-13,160** | 98 |
| Singida | 99,788 | 159,942 | **-60,154** | 60,946 | 104,820 | **-43,874** | 160,734 | 264,761 | **-104,028** | 61 |
| Tabora | 189,535 | 206,484 | **-16,949** | 107,032 | 135,322 | **-28,290** | 296,567 | 341,805 | **-45,238** | 87 |
| Tanga | 202,442 | 250,604 | **-48,162** | 224,785 | 164,237 | **60,548** | 427,227 | 414,842 | **12,385** | 103 |
| **JUMLA** | **4,141,250** | **4,961,076** | **-819,826** | **3,553,376** | **3,181,807** | **371,569** | **7,694,626** | **8,142,882** | **-448,256** | **94** |

| | 2002/2003 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Nafaka | | | MazaoYasiyo Nafaka | | | Jumla | | |
| Mkoa | | | Ziada/ Upungufu | Uzalishaji | Mahitaji | Ziada/ Upungufu | Uzalishaji | Mahitaji | Ziada/ Upungufu |
| Arusha | 258,200 | 372,708 | **-114,507** | 173,810 | 225,983 | **-52,174** | 432,010 | 598,691 | **-166,681** |
| DSM* | 7,724 | 388,322 | **-380,598** | 32,662 | 253,920 | **-221,258** | 40,386 | 642,242 | **-601,856** |
| Pwani * | 74,902 | 196,088 | **-121,186** | 254,135 | 119,047 | **135,088** | 329,037 | 315,135 | **13,903** |
| Dodoma | 262,952 | 268,635 | **-5,683** | 171,312 | 165,531 | **5,781** | 434,264 | 434,166 | **98** |
| Iringa | 402,226 | 273,218 | **129,008** | 161,736 | 168,904 | **-7,167** | 563,963 | 442,122 | **121,841** |
| Kagera | 126,817 | 277,064 | **-150,247** | 482,329 | 190,300 | **292,029** | 609,145 | 467,364 | **141,781** |
| Kigoma | 162,123 | 173,587 | **-11,464** | 154,371 | 121,898 | **32,473** | 316,494 | 295,485 | **21,009** |
| K’njaro | 195,677 | 217,071 | **-21,394** | 152,508 | 141,869 | **10,639** | 348,185 | 358,940 | **-10,755** |
| Lindi | 100,892 | 176,740 | **-75,848** | 171,644 | 81,525 | **90,119** | 272,537 | 258,265 | **14,271** |
| Mara | 190,571 | 222,625 | **-32,054** | 205,739 | 139,672 | **66,067** | 396,310 | 362,297 | **34,013** |
| Mbeya | 405,707 | 333,602 | **72,105** | 229,774 | 218,631 | **11,142** | 635,481 | 552,234 | **83,247** |
| Morogoro | 289,064 | 264,102 | **24,963** | 181,627 | 173,084 | **8,544** | 470,691 | 437,185 | **33,506** |
| Mtwara | 98,829 | 156,645 | **-57,816** | 304,784 | 102,659 | **202,125** | 403,613 | 259,304 | **144,308** |
| Mwanza | 325,577 | 394,740 | **-69,163** | 422,979 | 258,699 | **164,279** | 748,555 | 653,439 | **95,116** |
| Rukwa | 318,548 | 192,272 | **126,276** | 95,388 | 126,009 | **-30,621** | 413,936 | 318,281 | **95,655** |
| Ruvuma | 186,860 | 179,615 | **7,245** | 180,236 | 117,714 | **62,522** | 367,096 | 297,328 | **69,767** |
| S’yanga | 443,836 | 389,140 | **54,695** | 237,805 | 255,029 | **-17,224** | 681,641 | 644,170 | **37,471** |
| Singida | 166,912 | 163,940 | **2,972** | 109,554 | 107,441 | **2,114** | 276,467 | 271,381 | **5,086** |
| Tabora | 212,430 | 211,439 | **990** | 124,576 | 138,570 | **-13,994** | 337,005 | 350,009 | **-13,004** |
| Tanga | 210,771 | 255,867 | **-45,096** | 259,826 | 167,687 | **92,140** | 470,597 | 423,553 | **47,044** |
| **JUMLA** | **4,440,617** | **5,107,421** | **-666,804** | **4,106,795** | **3,274,172** | **832,623** | **8,547,412** | **8,381,593** | **165,819** |

- Kabla ya mwaka wa 2001/2002 takwimu za mikoa ya Pwani na Dar es Salaam zilikuwa zimeunganishwa.

*Chanzo: Wizara ya Kilimo na Chakula.*

**Kiambatanisho Na 3: Mpango wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika mabonde ya mito Pangani na Rufiji**

| BONDE | | SKIMU | Eneo (ha*) | Familia Zinazolengwa | Mazao | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Pangani | 1 | Mombo – Korogwe | 220 | 429 | Mpunga | Imekamilika |
| | 2 | Lekitatu – Arumeru | 464 | 235 | Mpunga | Imekamilika |
| | 3 | Soko – Moshi | 370 | 850 | Mpunga | Imekamilika |
| | 4 | Mahenge – Korogwe | 300 | 266 | Mpunga | Imekamilika |
| | 5 | Lemkuna | 430 | 402 | Mpunga, mahindi | Imekamilika |
| | 6 | Kambi ya Tanga - Arumeru | 410 | 490 | Mahindi | Imekamilika |
| | 7 | Kivulini – Mwanga | 410 | 400 | Mpunga, mahindi | Unaendelea kujengwa |
| | 8 | Longoi A - Hai | 300 | 400 | Mahindi, Maharage | Unaendelea kujengwa |
| Rufiji | 9 | Luganga – Iringa | 300 | 417 | Mpunga, mahindi | Imekamilika |
| | 10 | Ipatagwa I - Mbarali | 251 | 350 | Mpunga, mahindi | Imekamilika |
| | | Ipatagwa II | 291 | 370 | Mpunga, mahindi | |
| | 11 | Igomelo – Mbarali | 300 | 420 | Mpunga, mahindi | Imekamilika |
| | 12 | Ruanda Majenje – Mbarali | 450 | 560 | Mpunga | Imekamilika |
| | 13 | Mangalali – Iringa | 104 | 90 | Mboga | Imekamilika |
| | 14 | Mapagoro – Iringa | 350 | 150 | Mpunga, mahindi | Unaendelea kujengwa |
| | 15 | Nyamahana Iringa | 109 | 90 | Mpunga | Unaendelea kujengwa |
| **JUMLA** | | | **5059** | **5919** | | |

*Chanzo: Wizara ya Kilimo na Chakula*

* Eneo la skimu zilizokamilika ni hekta 3,890 na Familia zinazonufaika na skimu hizo ni 4,879

**Kiambatanisho Na. 4: Teknolojia zilizotolewa na vituo vya utafiti mwaka wa 2001/2002**

| Kituo | Teknolojia | Sifa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| **UKIRIGURU** | Aina 4 za mbegu bora za muhogo | Zinavumilia ugonjwa wa batobato na kutoa mavuno ya tani 10 hadi 40 badala ya tani 5 kwa hekta | Mbegu 249,000 zimesambazwa kwa wakulima wa Kagera, Mwanza na Mara. |
| **UYOLE** | Mbegu chotara ya mahindi aina ya UH 615 | Inavumilia ugonjwa wa ukungu wa mahindi (*Grey leaf spot*) na kutoa mavuno ya tani 8 kwa hekta badala ya tani tatu hadi nne kwa hekta | Tani 120 za mbegu zimezalishwa msimu huu ambapo tani 70 zilinunuliwa na wakulima wa mikoa ya Rukwa na Ruvuma. |
| | Aina mbili za mbegu za maharage UY96 na UY98 | Uwezo wa kutoa tani 2 hadi 2.5 kwa hekta | Mbegu zinaendelea kuzalishwa kwenye mashamba ya wakulima wadogo. |
| **SELIAN** | Aina mbili za mahindi za Situka M1 na Situka 1 | Zinastahimili ukame na kustawi kwenye ardhi ya rutuba ndogo | Uzalishaji mbegu mama umeanza. |
| | Aina 2 za mbegu za mahindi za Lishe M1 na Lishe1. | Zina lishe bora ya viini vya protini na hivyo zitasaidia kupunguza utapiamlo wa watoto. | Zinaendelea kuzalishwa kwenye vituo vya utafiti. |
| **KATRIN IFAKARA** | Aina 2 za mbegu bora za mpunga TXD85 na TXD88 | Zinatoa mavuno ya tani 6 hadi 8 kwa hekta badala ya tani 3. Zina ladha nzuri. | Uzalishaji mbegu unaendelea. |
| **ILONGA** | Aina 4 za mbegu bora za kunde | Zinakomaa mapema siku 60 badala ya siku 90-110. | Zinaendelea kuzalishwa kwenye mashamba ya wakulima. |
| **NALIENDELE** | Mbegu 2 bora za ufuta, Naliendele 92 na Ziada 94. | Zinazaa tani 1 kwa hekta badala ya tani 0.3 kwa hekta. | Zinaendelea kuzalishwa kwenye mashamba ya wakulima. |

*Chanzo: Wizara ya Kilimo*

**Kiambatisho Na.5: Mchanganuo wa Matumizi hadi tarehe 30 Juni 2002**

| ENEO | Kiasi Kilichoidhinishwa 2001/2002 (SH.) | Kiasi Kilichotolewa Hadi Juni 2002 (SH.) | Asilimia ya Kiasi Kilichotolewa /Kiasi Kilicho-idhinishwa | Kiasi Kilichotumika Hadi Juni 2002 (SH) | Asilimia ya Matumizi/ Kiasi Kilichotolewa |
|---|---|---|---|---|---|
| Mishahara na Marupurupu | 3,828,451,500 | 2,957,985,533 | 77.3 | 2,957,985,533 | 100 |
| Idara | 2,229,569,500 | 2,229,569,500 | 100 | 2,228,707,243 | 99.9 |
| Michango ya Kimataifa | 412,840,000 | 412,840,000 | 100 | 412,840,000 | 100 |
| Ruzuku kwa Mashirika | 855,766,000 | 855,766,000 | 100 | 855,766,000 | 100 |
| Mfuko wa Pembejeo | 456,730,000 | 456,730,000 | 100 | 0 | 0 |
| SGR | 1,572,450,000 | 1,572,450,000 | 100 | 1,572,450,000 | 100 |
| **JUMLA** | **9,355,807,000** | **8,485,041,033** | **90.7** | **8,484,178,776** | **99.9** |

**Jedwali Na.6: Kanda za Uzalishaji na mazao ya kupewa kipaumbele**

| Na. | Kanda | Mikoa | Mazao ya Kupewa Kipaumbele |
|---|---|---|---|
| 1 | Kanda ya Mashariki | Dar es Salaam, Tanga, Pwani na Morogoro | Mahindi, mpunga, minazi, miwa, mbaazi, korosho, mikunde, pamba, mkonge, viungo na matunda |
| 2 | Kanda ya Ziwa | Mwanza, Mara, Kagera na Shinyanga | Mahindi, muhogo, viazi vitamu, mpunga, maharage, mtama, ulezi, dengu, migomba, tumbaku, chai, kahawa na pamba |
| 3 | Kanda ya Kaskazini | Arusha, Kilimanjaro na Manyara | Mahindi, ngano, maharage, migomba, viazi mviringo, mtama, mbaazi, kahawa, pamba, pareto, shairi, vitunguu, mboga mboga na matunda |
| 4 | Kanda ya Kusini | Mtwara na Lindi | Korosho, ufuta, alizeti, minazi, muhogo, mtama, mahindi, mpunga, uwele na matunda |
| 5 | Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | Mbeya, Rukwa, Iringa na Ruvuma | Mahindi, mpunga, maharage, ulezi, alizeti, viazi, migomba, mboga mboga, pareto, kahawa, chai, tumbaku na matunda. |
| 6 | Kanda ya Magharibi | Tabora na Kigoma | Mahindi, mpunga, karanga, tumbaku, kahawa, pamba na michikichi |
| 7 | Kanda ya Kati | Dodoma na Singida | Mtama, uwele, karanga, vitunguu, mahindi, muhogo, pamba, zabibu, alizeti na tumbaku. |

*Chanzo: Wizara ya Kilimo na Chakula.*

**Kiambatanisho Na 7: Miradi ya umwagiliaji maji mashambani itakayotekelezwa mwaka 2002/2003**

| | JINA LA MRADI | MHISANI | KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA | MAHALI/SKIMU HUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mradi wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji katika Mabonde ya mto Pangani na Rufiji na Kuboresha Miradi ya Wakulima wadogo. | Mkopo kutoka Benki ya Dunia | - Kukamilisha ujenzi wa skimu nne (4) | - Longoi (hekta 300), Mapogoro (hekta 350), Kivulini (hekta 410) na Nyamahana (hekta 109). |
| | | | - Kuanzisha mashamba ya mifano katika skimu tatu (3) | - Longoi, Mapogoro na Kivulini. |
| | | | - Kuzalisha mbegu za mpunga katika skimu nne (4) | - Lekitatu, Igomelo, Luganga na Momba |
| 2 | Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo (ASPS) | Msaada kutoka Serikali ya Denmark | - Ujenzi wa miradi miwili (2), | - Lumuma (hekta 960) na Nyanzwa (hekta 760) |
| | | | - Kutoa mafunzo juu ya Umoja wa Umwagiliaji | - Lumuma (hekta 960) na Nyanzwa (hekta 760) |
| | | | - Kuandaa taratibu za wakulima kuchangia ujenzi katika skimu tatu (3) | - Lumuma (hekta 960), Nyanzwa (hekta 760) na Irindi (hekta 610) |
| | | | - Kuandaa mwongozo wa huduma za ugani | - Lumuma (hekta 960) na Nyanzwa (hekta 760) |
| 3 | Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani (PIDP) | Mkopo kutoka IFAD | - Kuunda na kuimarisha vikundi vya umwagiliaji | Eneo lote la mradi, lenye skimu 18 (hekta 3,900) |
| | | | - Kujenga skimu za umwagiliaji na visima vifupi | |
| | | | - Kuendeleza ujenzi wa visima vifupi na skimu za umwagiliaji | |
| 4 | Mradi wa Umwagiliaji Maji Mashambani Lower Moshi (Awamu ya Pili) | Msaada kutoka Serikali ya Japan | - Kuweka utaratibu wa mgawanyo wa maji kwa watumiaji mbalimbali, | Lower Moshi (hekta 2,400) |
| | | | - Kuandaa mpango kazi wa utekelezaji. | |
| 5 | Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji Maji Mashambani (NIMP) | Msaada kutoka Serikali ya Japan | Kukusanya na kufanya uchambuzi wa takwimu na taarifa za miradi na kuainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. | Nchi nzima |
| 6 | Ukarabati wa Skimu za Umwagiliaji maji zilizochakaa | Serikali ya Tanzania | - Kukarabati miundombinu ya skimu saba (8). | Mvumi – Kilosa (hekta 260), Musa – Hai (hekta 641), Katuka – Sumbawanga (hekta 100), Muhwazi – Kibondo (hekta 100), Bugorora – Ukerewe (hekta 200), Kalemela – Magu (hekta 20) Mbarika – Misungwi (hekta 45) na Kalenga, Iringa (hekta 240) |
| | | | - Kuanzisha vyama vya umwagiliaji katika skimu tano (5) zilizokamilika. | Buswahili – Musoma, Balili – Bunda, Ochuna – Tarime, Lumuma – Kilosa, Ruvu – Kibaha na Bagamoyo. |

*Chanzo: Wizara ya Kilimo na Chakula*

**Kiambatanisho Na. 8: Mpango wa kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji katika Programu husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji (PIDP)**

| Wilaya | Skimu |
|---|---|
| Babati | Mawe Mairo/Mafuta<br>Gichameda<br>Quash |
| Dodoma | Mpwayungu<br>Mtitaa<br>Uhelela |
| Kwimba | Kimiza<br>Luhala<br>Shilanoma |
| Manyoni | Udima<br>Mwiboo<br>Msemembo |
| Nzega | Chamipula<br>Lukui<br>Sigiri |
| Shinyanga | Nyida<br>Itilima<br>Bubale/Masegwa |

*Chanzo: Wizara ya Kilimo na Chakula*